# *Thibitisho La Kufufuka Kwake*

Asante, Ndugu Neville. Habari ya asubuhi, marafiki. Ni vizuri kuwa hapa maskanini tena asubuhi ya leo, kumwabudu Bwana Yesu. Hii ni ibada yetu ya pili kwa wengi wetu, leo. Tulikuwa hapa mapema, asubuhi ya leo, naye Bwana akakutana nasi kwa njia ya ajabu. Nami nilikuwa nishuke nije kuzungumza tu na hawa jamaa kwa dakika chache, wala hata sikutarajia kuwa na somo. Na, muda si muda mwajua, nikaanza kuhubiri. Na hapo tulikuwa na wa—wakati mzuri sana, nasi tunamshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hili.

2 Sasa, tunasikitika, katika maskani hii ndogo hapa hatuna nafasi ya kuketi kwa watu ambao inawabidi kusimama hivyo. Nachukia hili, vibaya sana, lakini ndiyo yote tunayoweza kufanya kwenye wakati huu. Kwa hiyo tutajaribu kutowashikilia kwa muda mrefu sana; salamu ndogo tu za Pasaka kwenu nyote. Nasi tutawaombea wagonjwa, asubuhi ya leo, kama ilivyotangazwa. Na Bwana na aongeze baraka Zake kwa kila jambo tufanyalo, kwa sababu tuko hapa kwa kusudi hilo, kwamba Mungu atakutana nasi na kutubariki.

3 Sasa, ibada ya usiku wa leo ni ibada ya ubatizo. Nanyi ambao bado hamjabatizwa kwa kuzamishwa, na mnatamani kufanya hivyo, mbona, tungewaalika hapa usiku wa leo. Njoni, mkiwa tayari, na mlete mavazi yenu ya ubatizo, kwa maana tunatarajia ibada kubwa hapa usiku wa leo, katika njia ya ubatizo.

4 Na sasa, leo, kwa kuwa ni Pasaka, na wengi wenu tayari mmekuwa, pengine, kwenye ibada zenu wenyewe, au hapa kwa ibada ya mapambazuko. Tuna furaha kuwa nanyi humu katika sehemu hii ya . . . ya ibada yetu leo.

5 Lakini kuendelea kwa ajili ya mazungumzo mafupi ya Pasaka, asubuhi ya leo, tungeelekeza usikivu wenu kwenye Injili ya Yohana Mtakatifu, mlango wa 21, na kifungu cha 3 na cha 4. Na kisha katika Marko Mtakatifu . . . au Luka Mtakatifu, hasa, mlango wa ishiri- . . . au wa 49. Ningependa kusoma kwa dakika chache tu. Kwanza, Yohana Mtakatifu 21.

*Simoni Petro akawaambia, Naenda kuvua samaki. Nao wakamwambia, Sisi nasi pia tutakwenda nawe. Wakatoka, wakapanda chomboni mara; ila usiku ule hawakupata kitu.*

*Hata asubuhi kulipokucha . . . Yesu alisimama ufuoni: walakini wanafunzi hawakujua ya kuwa ni Yesu.*

6 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye sehemu hiyo ya Neno. Halafu, katika Luka 49. . .mlango, na kuanzia kifungu cha 27.

> *Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza. . .maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.*
>
> *Wakakikaribia kile kijiji walichokuwa wakienda: naye alifanya kama anataka kuendelea mbele* kidogo.
>
> *Lakini wakamsihi, wakisema, Kaa pamoja nasi: kwa kuwa kumekuchwa, na mchana umekwisha. Akaingia ndani kukaa nao.*
>
> *Ikawa* walipokuwa *ameketi nao chakulani, alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa.*
>
> *Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua;. . .*

7 Ni tofauti jinsi gani! Mahali pamoja hawakumtambua. Na mahali hapa, walimtambua, kwa jambo fulani alilofanya.

> *. . .kisha akatoweka mbele ya macho yao.*
>
> Wakaja *wakaambiana, Je,* mioyo *yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na. . . ametufunulia maandiko?*

8 Sasa na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda mfupi tu wa maombi.

9 Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, tunakushukuru, asubuhi ya leo, kwa tukio hili kuu tulilo nalo, kukusanyika pamoja Mbele za Kristo, kwenye ufufuo; kuwa na hakikisho hili kamilifu ya ushirika wa Kiungu, washiriki wa kusulubishwa Kwake, kusulubishwa pamoja Naye kwa mambo ya ulimwengu, na kufufuka upya tena kwa Uzima wa Milele. Nalo tumaini hili liko ndani yetu sasa.

10 Na kama yule nabii wa kale, tunasema, "Tunajua Mkombozi wetu yu hai." "Anaishi milele, ameketi mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu; Kuhani Mkuu anayestahili, Yule ambaye ameonja mateso na anaweza kufanya maombezi juu ya maungamo yetu." Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa hili! Mioyo yetu inawaka ndani yetu tunapofikiri kwamba tunaye Mtu anayetuwakilisha, leo hii, Mbele za Mungu mkuu na Mwenyezi. Yeye hajafa, bali yu hai, na ameketi katika Uwepo Wake. Naye yupo kabisa, kila mahali, anajua mambo yote, mwenye uwezo wote, anaweza kufanya mambo yote, anajua mambo yote, naye yuko daima. Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya Kweli hii kuu na tukufu ambayo tunashikilia vifuani mwetu leo, tunaithamini sana!

11 Na, Mle ndani, anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, kwa maana aliteseka kwa ajili yetu, akichukua magonjwa yetu pale Kalvari. Tuna furaha sana kwa hilo, kujua hilo leo,

na kujua hakikisho la moja kwa moja tulilo nalo sasa. Yeye yu hai, akizungumza kwa ajili yetu, akitupenda. Hivi hutaruhusu Uwepo Wake uendelee pamoja nasi leo, uifanye kuwa Pasaka halisi!

12 Na, Mungu, kwa wale wasiokujua asubuhi ya leo, ambao ni wageni, hawamjui Kristo katika ufufuo, tunaomba kwamba atakuja katika uwezo mkuu kamili, akiondoa dhambi za maisha yao na kuwapa vitu vyema vya Mungu, badala yake. Lijalie, Bwana. Jalia siku hii ilete hilo kwa kila asiyeamini aliye katika Uwepo wa Kiungu.

13 Bariki ibada zote katika nchi zote, zinazofanyika leo katika kumbukumbu ya ukumbusho huu mkuu.

14 Sasa msaidie mtumishi Wako asiyefaa, Bwana, tunapojikabidhi Kwako. Bariki kila mtu aliye hapa. Na jalia, ibada itakapokwisha, na tuseme kama wale huko Emau siku ile, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?" Tujalie, Bwana, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

15 Katika majaliwa ya mpango mkuu wa Milele wa Mungu wa wokovu, jinsi ambavyo katika nyakati zilizopita, Mungu alipomfanya mwanadamu awe anamwabudu Yeye, alimfanya hivyo, ili aweze kumwabudu. Aweze kuwa na shauku ya kuabudu. Na kote katika nyakati, mwanadamu ametamani kutazama ng'ambo ya pazia linaloning'inia kati yake na anakokwenda.

16 Katika mwaka wa 603 A.D., wakati mfalme wa Uingereza alipobatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo, na Mtakatifu Augustino. Wakiwa wameketi mekoni usiku mmoja, alipokuwa akizungumza naye juu ya Kristo, shomoro mdogo aliruka ndani ya huo mwanga, akapapatika kidogo, akaondoka. Ndipo Mtakatifu Augustino akamwambia mfalme, akasema, "Alitoka wapi, na alienda wapi?" Akasema, "Hiyo ndiyo njia ya kila mtu anayekuja katika ulimwengu huu. Anaingia humu, anatembea katika dhamiri ndogo ya hisia, bila kujua alikotoka hasa. Na kuna Kitabu kimoja tu kinachoweza kumwambia anakoenda, na hicho ni Biblia." Na, kwa jambo hilo, huyo mfalme aliongoka na kutoa maisha yake kwa Bwana. Na, kesho yake asubuhi, yeye na nyumba yake yote walibatizwa katika Jina la Bwana.

17 Mwanadamu katika hali yake ya asili, hawezi—hawezi kuelewa mambo ya kiroho. Yanatambulikana kiroho.

18 Na sasa nataka msikilize kwa makini mwezavyo. Najua ni ngumu, huku mmesimama, na kusongamana jinsi kusanyiko lilivyo. Lakini jaribuni kusikiliza Neno, kwa ajili ya wale walio wagonjwa na wale walio wagonjwa wa dhambi; hasa kwa wale ambao ni wagonjwa wa dhambi, asubuhi ya leo, na wanataka kupata amani.

19 Tangazo la ukombozi limetiwa saini. Uko huru, nawe hujui tu. Lakini, imani haina budi kuwa na mahali pa Kiungu pa kutulia, hapo kabla. Kama unamwamini Mungu, huna budi kuwa na mahali pa Kiungu pa kupumzikia pa kuiweka. Wala hakuna mahali pazuri zaidi, na hakuna njia nyingine ya Kiungu, ila kupitia Neno takatifu la Mungu. Nasi tunataka kuacha imani yetu ikae moja kwa moja juu ya Neno la Mungu lililoandikwa.

20 Sasa, mwanadamu, katika hali yake ya kimwili na mawazo yake ya kiakili, yeye sikuzote hujiondoa kwa Mungu. Imekuwa, tangu mwanzo, kwamba mwanadamu anatamani kuona ng'ambo ya pili, lakini amefungwa katika nyumba ya gereza. Wakati mwingine mapokeo ya mwanadamu yanamweka humo, ambapo wanafundisha mapokeo ya aina mbalimbali na nia za jinsi ya kuabudu. Naye anawaweka watu chini ya utumwa, chini, katika mapokeo yake. Na hiyo imekuwa tangu ulimwengu ulipoanza. Imekuwa hivyo. Naye amefungwa katika—katika nyumba za magereza.

21 Lakini mwanadamu daima ametamani kuona ng'ambo ya pili. Na kitu chochote kidogo kinachoonekana kuwa cha kimbinguni kidogo, mwanadamu atakikimbilia, kwa sababu ni namna fulani ya ahadi upande mwingine wa mpaka, upande wa pili wa njia. Na kinachomfanya afanye hivyo ni kwa sababu ameumbwa kwa mfano wa Muumba wake, Mwenyezi Mungu. Ameumbwa apate kumwabudu Mungu, naye hana budi kutafuta mahali pa kutolea hisia hiyo.

22 Na hilo ndilo kusudi letu hapa leo, katika asubuhi hii ya Pasaka, ni kuwasilisha kwenu Ukweli halisi wa Injili. Hakuna kitu ndani ya mtu yeyote, juu ya shirika lolote, juu ya msingi wowote; ni juu ya Injili tu, Kweli rahisi za Biblia. Ninaamini ya kwamba ni Neno la Mungu lililoandikwa. Ninaamini kwa nafsi yangu yote, moyo, akili, na utu wangu wote. Na hilo ndilo ninalotaka kuwasilisha kwa huu, maskini mji wetu hapa leo, katika jambo hili kuu la ajabu ambalo nimeliona likitendeka duniani kote kwa miaka kumi iliyopita.

23 Tulijaribu, mara nyingi, kufanya ibada, ibada za uponyaji, mjini; si kwa sababu nafikiri sina marafiki hapa. Kwa sababu, ninao marafiki. Nanyi ni marafiki zangu, nami nawapenda. Lakini ni wazo kwamba hapa ni nyumbani, ambapo nililelewa. Ni mahali pangu, ambapo kila mtu ananijua hapa, na kwa hivyo kidogo inaifanya kuwa ngumu. Maana, Maandiko yalisema jambo lile lile, ya kwamba, "Katika mji wako mwenyewe, au miongoni mwa watu wako mwenyewe," na kadhalika, ni vigumu zaidi kuiwasilisha Injili. Imekuwa hivyo, katika nyakati zote, nao huu haungekuwa tofauti sasa.

24 Lakini, ninaamini, kwa moyo wangu wote, ya kwamba Mungu atatuhusu tuwe na ibada asubuhi ya leo kama tulivyomwomba afanye. Sasa, ninaamini ya kwamba atafanya

jambo hilo. Kwa hiyo, iwapo atafanya hivyo, kwa Uwepo Wake mkuu na uweza Wake, hiyo inamaanisha basi kwamba Yeye yuko mbele zetu. Na ni wakati wa ajabu jinsi gani, kwenye asubuhi ya Pasaka, kumwona Bwana Yesu aliyefufuka akitembea miongoni mwa wanadamu, akitembea hapa, kama thibitisho lisiloweza kukosea, lisilofutika kwamba kweli Yeye alifufuka kutoka kwa wafu.

25 Na hizi ndizo hoja zangu, ndizo nimekuwa nikishindania, kwamba Yesu hajafa. Yeye yu hai, yu hai kabisa, na atakuwa hai, milele na milele. Na kama Mungu ataturuhusu tu, kwa neema Yake, naamini, asubuhi ya leo, ya kwamba tunaweza kuwathibitishieni, bila shaka lolote, kwa msaada wa Roho Mtakatifu, kwamba Yesu kweli alifufuka katika wafu, naye yu hai papa hapa leo, akiishi papa hapa jengoni, pamoja nasi. "Hata ukamilifu wa dahari." Aliahidi hilo.

26 Sasa, mwanadamu, kwa njia yake ya kimwili, amejenga kwanza. . .Tutaona kuwa watu, kwa nia njema, wanajaribu kuishusha Injili ikawa kanuni ya imani, wanajaribu kusema, "Vema, tutaenda kanisani." Hilo ni jema. Na kwa nia njema, wanasema, "Tutakuwa na aina *hii* ya a—azimio la kanuni ya imani. Tutakariri sala hizi. Tutafanya jambo fulani." Lakini kufufuka kwa Kristo kunajumuisha zaidi ya kanuni za imani, zaidi ya dhehebu. Ingawa, kadiri zinavyoweza kuwa nzuri, na nia ni nzuri, lakini huyo siye Kristo aliyefufuka.

27 Na hilo ndilo jambo kuu tunalofuata, asubuhi ya leo, ni thibitisho lisiloweza kukosea kwamba Yesu alifufuka katika wafu.

28 Sasa, kama somo letu linavyosema, "Hawakumtambua," na ni jambo lile lile leo.

29 Lakini mwanadamu ametamani kumjua. Kote katika wakati, wametamani kumjua. Na somo letu asubuhi ya leo, ninii letu. . .*Mkombozi Wangu Yu Hai*, katika ibada ya mapema Jumapili, tunaona hapo ya kwamba Ayubu, kadiri alivyokuwa mzee, na huko nyuma kabisa kwanza, mwanzoni, alitamani kumjua Muumba wake. Kwa maneno mengine, alisema, "Laiti ningeliweza kwenda na kubisha mlangoni Pake na kuzungumza Naye!" Jinsi moyo wa mwanadamu umetamani sana mambo kama hayo! Na leo hii, baada ya miaka elfu nne, karibu elfu tano zaidi, ni zaidi sana vipi moyo wa mwanadamu siku hizi unatamani kwenda mlangoni Pake, kubisha mlangoni Pake, kumfahamu!

30 Halafu basi, watu, kupitia mapokeo, wamewapofusha watu kutoka kwenye zile Kweli kuu za msingi za Maandiko.

31 Sasa, Yesu alinena jambo lile lile alipokuwa hapa duniani. Alisema, "Nyinyi ni viongozi vipofu wa vipofu." Alisema, "Kipofu akimwongoza kipofu, si wote watatumbukia shimoni?"

32 Sasa, kuwaita walimu wa Kikristo au wa kidini "vipofu." Mnaona? Mungu anayo njia ya kujidhihirisha Mwenyewe kwa watu, na kujitambulisha Mwenyewe kwa watu. Lakini, mara nyingi, mapokeo yanawafungia watu kabla Mungu hajapata nafasi ya kuingia ndani yao, kujifunua Mwenyewe. Mnaona? Mnalipata? Mnaona? Mapokeo! Loo, jinsi hayo yalivyo siku hizi!

33 Sasa, wale walimu ambao Bwana Yesu alikuwa akiwazungumzia, walikuwa wa kimsingi sana. Walikuwa wasomi kwelikweli. Walishika andiko la Neno, torati, kikamilifu; hakuna yodi moja au nukta, wala chochote kile, kingepita kutoka humo. Na lazima wawe nalo kikamilifu.

34 Kwa hiyo, tunaweza kuwa wakamilifu sana kwa elimu yetu na kwa nadharia yetu mpaka tunamwacha Kristo nje ya picha kabisa. Tunaenda mbali kutoka kwenye kweli halisi.

35 Sasa, kwa hiyo, ili kuifikisha Kweli kwa mwanadamu, kwa Mungu, "Mungu alimtuma Mwanawe Mwenyewe, aliyefanywa kwa mfano wa mwili wenye dhambi," Naye akazaliwa hapa duniani. Naye alikuwa u—upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, akatolewa siku ya Kal-. . . pale Kalvari, kuziondoa dhambi zetu; na kutupa uhuru, na kututoa katika magereza tuliyokuwamo.

36 Sasa, mwanadamu ni mfungwa. Mungu alisema kwamba mwanadamu alikuwa mfungwa, kwa hiyo, mpaka jambo fulani limemtokea huyo mtu. Nawatakeni mpate jambo hili sasa. Kwamba, kabla ya jambo hili fulani, linaloitwa Kuzaliwa upya, halijamtokea mwanadamu huyo, hawezi (hakuna njia, hata kidogo) kuelewa, au kumwelewa Mungu kamwe, au kuwa na maarifa yoyote ya Mungu. Ingawa Neno linalinena, akili yake haiwezi kulifahamu, kwa maana ni akili ya mwanadamu. Hana budi kuwa na nia ya Mungu ndani yake, apate kuelewa mambo ya kiungu. Mnaona? Kwa hiyo, usomaji wote, shule zote, mafundisho yote, kadiri yawezavyo kuwa mazuri, hata hivyo hiyo siyo kanuni halisi bado.

37 Mungu alimtuma Mwanawe, akihubiri Injili. Hiyo ni kweli. Injili ni habari njema. Katika Isaya 61, kwenu ninyi mnaoandika Maandiko, Mungu alisema pale, akinena. . . Isaya, hasa, juu ya kuja kwake Kristo. Alisema, "Mungu amenitia mafuta kuhubiri Injili, kuleta habari njema; na kuwafungua wafungwa, na kufungua milango ya gereza, na kuwaweka wafungwa huru." Mungu alimtuma Kristo kufungua milango ya gereza ya watu wanaokaa gizani. Na kama ukiangalia wa—wale aliozungumzia, "kuwaweka huru," haikuwa wale wasiojua kusoma na kuandika. Ilikuwa ni wasomi, wale wenye elimu, Kristo alikuja kuwaweka huru.

38 Sasa ili kulifanya hivi kwamba watoto wadogo wangeelewa. Kristo alipokuja. . . Tuseme, kwa mfano, leo hii, kwamba kila mmoja wenu alihukumiwa kifo. Nawe ulikuwa umeketi gerezani,

ukijua ya kwamba, jua likichomoza kesho asubuhi, ulipaswa kufa.

39 Na wengi wenye dhambi, na walio mbali na Mungu, wameketi mahali hapo asubuhi ya leo. Watu wengi, ambao ni watu wazuri kweli, wameketi katika hali hiyo asubuhi ya leo.

40 Wengi wenu, wanaoketi hapa na kansa, na uvimbe, na upofu. Baadhi yenu, mlioketi katika hali ya kila namna. Hata hivyo, Mungu alimtuma Kristo kufungua milango ya gereza, kukuweka huru. Unasema, "Kwani ugonjwa ni utumwa?" Naam.

41 Yesu alilielezea waziwazi, alipomwambia yule mwanamke aliyekuwa amepinda. Akamponya; akaweka mikono Yake juu yake, naye akanyoka. Ndipo wakaanza kutafuta makosa, hao walimu wakatafuta. Akasema, "Je, haikumpasa binti huyu wa Ibrahimu kufunguliwa, kuwekwa huru na kifungo hiki ambacho amekuwa nacho, cha Shetani?"

42 Kwa hiyo, Kristo Mkombozi wetu mkuu amekuja kuwaweka huru wanaume na wanawake kutoka kwa dhambi, na huru na magonjwa. Yeye, alipokufa pale Kalvari, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa."

43 Sasa, hiyo ndiyo habari njema. Hiyo ndiyo Injili. Injili ni, kwamba, Kristo alikufa mahali pa mwenye dhambi, kwamba Kristo alichukua mahali pa mgonjwa. Kristo alichukua mahali pa mwenye dhambi. Kristo alichukua mahali pa mtu mwenye wasiwasi. Kristo alichukua mahali pa mwendawazimu. Kristo alichukua kila mahali, na akatuweka huru na kila dhiki na kila dhambi ambayo shetani alituwekea gerezani. Kristo alikuja kutusamehe, bure. Kila kitu kinatolewa bure.

44 Katika zile siku ambazo watumwa, wakati walipokuwa utumwani, nao walikuwa watumwa hapa Marekani. Wakati Abraham Lincoln alipofariki, kumweka huru mtu mweusi, kumpa haki asiwe mtumwa tena, waliwekwa huru machweo, pia. Walilifurahia sana, wakijua kwamba walikuwa wanaenda kuwa huru mara tu jua likichomoza. Baadhi yao ambao walikuwa na afya njema zaidi, wazima zaidi kimwili, walipanda juu sana mlimani. Wengine wangeweza kupanda hata kwenye kilele; na wengine kupanda kufikia nusu; na wengine chini kabisa. Basi mara jua lilipoanza kuchungulia, wale wakubwa wenye nguvu walikuwa huko juu.

45 Ningefananisha hilo leo na Wakristo wakuu wenye nguvu wanaoinuka katika nyanja za Roho Mtakatifu; wale wanaokuja tu njiani chini ya kuhesabiwa haki; wale walio chini kabisa katika bonde la kuchanganyikiwa.

46 Wakaamka. Na mara wale, waliokuwa juu, waliweza kuliona, kwanza, kwa mbali kabisa. Ndipo walipoliona jua likichomoza, walipiga kelele kwa sauti zao zote, kwa wale waliokuwa chini yao, kasema, "Tuko huru!"

47 Ndipo hao nao wakalipata, na kuwapigia makelele na mayowe hao wengine waliokuwa chini, "Tuko huru!"

48 Nao hao wengine, chini ya hao, wakawaelezea hao wengine, "Tuko huru!"

49 Sasa tazameni. Wale walio juu ya kilima wangeweza kuliona jua, kwa hiyo walikuwa huru. Lakini mara tu habari zilipomjia yule jamaa bondeni, alikuwa huru tu kadiri alivyoweza kuwa, kama jua lilikuwa limechomoza au la. Mnaiona?

50 Kristo alikuja kuwaweka huru mateka. Sio lazima ufungwe na tabia, maisha ya nusu Ukristo. Mungu hataki uwe hivyo. Anataka uwe huru. Mungu alimtia mafuta Kristo kuhubiri uhuru, kufungua milango ya gereza. Na kila wakati unaponinii . . .

51 Tuseme umeketi mle ndani, na hukumu yako ya kifo iko juu yako. Ndipo muda si muda wajua, wanajitayarisha kukutoa nje wakakusulubishe, au kukuadhibu kwa njia fulani. Na jambo la kwanza, unamsikia mtu akishuka barabarani, akisema, "Acheni! Nina msamaha. Haikubidi kufa." Sasa, huna haja ya kungojea hadi utoke gerezani. Uko huru tu wakati huo kadiri utakavyokuwa utakapokuwa nje. Kwa hivyo mtu huyo anaweza kuwa na furaha tu, akiwa ameketi gerezani, kama vile angekuwa nje ya gereza, maadamu anajua msamaha wake umetiwa sahihi.

52 Ndivyo ilivyo asubuhi ya leo. Hii hapa! Kwa kila mwanamume na mwanamke ambaye ana moyo wenye njaa, kutoka katika vyumba vya magereza asubuhi ya leo, habari njema ya Injili inahubiriwa. Na haijalishi, ikiwa bado umekaa mgonjwa, ikiwa bado umekaa umefungwa, unaweza kuwa huru vile vile tu kwa sababu habari zimekuja, "Umesamehewa!" Kristo alifufuka, miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, asubuhi ya leo, kumweka huru kila mfungwa, akafungua milango ya gereza na kuwaruhusu watoke. Loo, ni jambo la ajabu jinsi gani!

53 Si ajabu mshairi alisisimkwa aliposikia hivyo! Uvuvio ukamshika, akasema:

> Alipoishi, alinipenda; alipokufa, akaniokoa;
> Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
> [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . huru milele:
> Siku moja yuaja—loo, siku yenye utukufu!

54 Matumaini ya mwaminio ni kutazamia kule Kuja mara ya pili, Mtawala huyu mkuu aliyefungua milango ya gereza na kutuweka huru. Deni imelipwa. Yote imelipwa. Mungu na wenye dhambi walipatanishwa pamoja pale Kalvari, Yesu alipokufa. Naye Mungu akamfufua siku ya tatu, kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu. Kwamba, tunapolitazama jambo hilo na kuliamini, na kulikubali kwa moyo wetu wote, tunahesabiwa haki

machoni pa Mungu aliye hai. Hakika inakufanya ushikwe na mhemuko! Bila shaka inakufurahisha! Ungewezaje kunyamaza? Mwanadamu angewezaje kujizuia, ambaye anajua ya kwamba kifo kinaning'inia pale mbele yake, na huu hapa msamaha unakuja? Hiyo ni kweli.

55 Unafikiri maskini Baraba alijisikiaje asubuhi ile, aliposikia Mrumi akija na ninii kubwa. . . kutoka kwenye orofa za juu? Huku viatu vikubwa vya chuma vikikanyaga, minyororo ikichacharisha, mkuki ukikokotwa barabarani; kujua kwamba atauawa, na . . . alipofungua mlango! Naye Baraba, akitetemeka na kulia, akiwa tayari kutoka mbio, akisema, "Loo, huu ndio mwisho wangu!"

Kasema, "Baraba, nilisoma, 'Umesamehewa, uko huru.'"

"Kwa nini," akasema, "sitakufa?"

Kasema, "Hapana. Si lazima ufe."

"Naam, ilinibidi kufanya nini kwa ajili yake?"

"Hakuna."

"Vema, hii inakujaje?"

56 Ndipo yule akida angemwinua hapo, aseme, "Unamwona yule Mtu anayening'inia pale msalabani? Unaona yale mate ya dhihaka kutoka usoni Mwake? Unaona yale majeraha mkononi Mwake? Hayo yalikuwa yako, lakini Yeye akapachukua mahali pako."

57 Alifungua mlango wa gereza kwa ajili yako, kusudi wewe, uliyehukumiwa kifo, Yeye amechukua mahali pako. Na kwenye asubuhi ya Pasaka, Mungu alimfufua kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu. Mbona, tumehesabiwa haki. Tunapoamini hii hadithi na kuikubali, amani ya kuhesabiwa haki inaingia ndani ya mioyo yetu, kama vile mawimbi yasiyopimika yanavyofingirika, jinsi mawimbi ya Utu Wake.

58 Mungu hakutuacha yatima. Alijua ya kwamba yote yangevurugika, katika siku zijazo; kupitia kwa walimu, na kadhalika, wa Neno, jinsi wangeweza kulichanganya. Lakini Yeye alimtuma Mjumbe wa moja kwa moja pamoja Nalo, Roho Mtakatifu, ambaye ni thibitisho la ufufuo.

59 Kama hakuna Roho Mtakatifu wa kuuthibitisha, basi singeweza kuuamini huo ufufuo; nisingekuwa na kitu ila theolojia; au nisingekuwa na kitu ila dhana ya kiakili. Lakini, siku hizi, haitubidi. . . Dhana ya kiakili ni sawa; theolojia ni sawa. Lakini tunaye shahidi wa moja kwa moja. Roho Mtakatifu ni shahidi wa ufufuo wa Bwana Yesu. Ameeleweka vibaya sana na watu siku hizi, katika siku zetu! Ameeleweka vibaya sana, lakini ndiye tumaini!

60 Wakati alipotoa agizo la mwisho pale, aliposema, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.

Aaminiye na kubatizwa ataokoka; na asiyeamini, atahukumiwa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Kwa Jina Langu watatoa pepo wachafu; watanena kwa lugha mpya; wakishika nyoka au vitu vya kufisha, havitawadhuru; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." "Mambo yale yale nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya, hata makubwa kuliko haya, kwa maana Mimi naenda kwa Baba Yangu."

61 Mtu fulani anasema, "Ndugu Branham, je, agizo hilo kuu lilifikia siku hii?"

62 Bila shaka. Umbali gani? "Ulimwenguni mwote." Wangapi? "Kwa kila kiumbe." Haya basi. Kuliamini, ni Uzima wa Milele, kulikubali.

"Kwa nini niliamini?" ungesema.

63 Kwa sababu, ni Neno la Mungu. Hiyo ni kweli. Mungu hawezi kulighairi Neno Lake Mwenyewe. Mungu anaponena Neno, hana budi kudumu Nalo. Ninaweza kusema neno, na kulighairi; unaweza kufanya vivyo hivyo. Lakini Mungu hawezi. Anaponena Neno, hana budi kudumu Nalo. Naye alisema Maneno hayo, kwa hiyo Mungu huliheshimu Neno Lake.

64 Nao ufufuo ni muhimu vivyo hivyo leo hii, na halisi tu vivyo hivyo kwa kila moyo wa mwanadamu unaoliamini, kama ilivyokuwa kwa Mariamu Magdalene na wale waliosimama kaburini asubuhi ile, waliomwona. Huyu hapa, na hapo jina lake likaitwa, "Mariamu." Naye akatazama pande zote na kusema, "Raboni," au, "Mwalimu!" Hiyo ni halisi kwa kila moyo asubuhi ya leo, ambao umezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, kwa nguvu za ufufuo, kama ilivyokuwa kwa yule mwanamke aliyesimama kaburini asubuhi hiyo.

65 Sasa, huwezi kulifanya kwa akili yako mwenyewe. Huwezi kulifanya. Wewe ni kama unajaribu kuweka karatasi kwenye jengo, au kulipaka rangi, wakati hali za mambo ni mbaya sana, wakati msingi umekataliwa.

66 Kama serikali ikiikataa nyumba, misingi imeoza, unawezaje kujenga juu ya nyumba hiyo? Unajenga tu ipate kuanguka. Haijalishi unapaka rangi ndani jinsi gani, unaweka karatasi nzuri jinsi gani juu yake, unaweka viezekeo vingapi juu yake, unainua madhabahu mangapi, umeweka misalaba mingapi ndani yake, haina budi kuanguka, kwa maana msingi ni mbaya. Msingi umeoza.

67 Naye mwanadamu, kwa njia yake ya kuwazia kiakili, kwanza kabisa amekosea. Yeye ni mgeni mbali na Mungu. Amekatiliwa mbali, bila tumaini, bila Mungu, bila huruma.

68 Na jambo pekee analoweza kufanya ni kuja na kumkubali Kristo. Ndipo Roho Mtakatifu anaingia, nayo nia iliyokuwa ndani ya Kristo iko ndani yako.

69 Yesu alisema, "Baba, aliyenituma, yuko pamoja Nami." Loo, jamani! Ni tangazo la jinsi gani! Neno la jinsi gani! "Baba, aliyenituma, anakuja pamoja Nami."

70 Sikilizeni! "Na kama vile Baba alivyonituma Mimi, Mimi nami nawatuma ninyi." Si kwamba tu anakutuma, bali anaenda nawe. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Yote yaliyokuwa ndani ya Mungu yalimiminwa ndani ya Kristo; na yote yaliyokuwa ndani ya Kristo yalimiminwa ndani ya mwaminio, Kanisa. Mungu yu pamoja nanyi. "Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari." Hilo ndilo tangazo la Neno la Mungu. Hivyo ndivyo Biblia inavyosema. Hilo ndilo ninaloamini.

71 Na kama ikitubidi kulisimamia peke yetu, simama, kwa sababu ni Neno la Mungu. Kila mtu aliyepata kufikia popote, ilimbidi asimame, peke yake, juu ya imani yake pekee. Hilo halipo kwenye ushirikiano. Kuna Mmoja tu ambaye atatembea pamoja nawe, na huyo Ndiye aliyetoa tamshi hilo. Bwana Yesu, Ndiye ambaye ametembea bondeni pamoja nawe. Atapitia katika kila sehemu yenye michongoma na kupanda kila mlima, kando yako.

72 Jifunge nira pamoja Naye. "Kwa maana nira Yangu ni nyepesi, na mizigo Yangu ni rahisi." Usifungwe nira pamoja na mambo ya dunia. Usifungwe nira katika mashirika na madhehebu mbalimbali. Jifunge nira peke yako pamoja na Bwana Yesu Kristo, ni utaratibu kwamba unaweza kufanya hivyo. Amini, na uone ufufuo.

73 Basi, mitume hawa, wakiwa wangali ni watu waliotembea pamoja na Yesu, waliokuwa na ushirika Naye, walitembea katika hali ya kawaida, kama wanadamu siku hizi. Lakini walishindwa kutambua Yeye alikuwa ni Nani.

74 Yesu alisema, "Enyi Mafarisayo vipofu." Alisema, "Loo, mnazichukua amri za Mungu," angalieni, "na kuzitangua kwa mapokeo yenu." Mnaona?

75 Hao hapo, walimu, wanachuoni, wanafunzi wa seminari! Nayo Maandiko yalisema waziwazi ya kwamba Yesu angekuja jinsi alivyokuja, lakini mapokeo yao hayakulifundisha hivyo. Walijaribu kulisugulia mbali, na kusema, "*Huo* ulikuwa ni wakati mwingine. Nao *Huu* utakuwa ni wakati mwingine." Lakini Mungu alikuja vile vile tu.

76 Na, siku hizi, kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo sasa. Wanaweka sehemu *hii*, kando, na sehemu *hii* kando, na kusema, "Mungu alitenda wakati huo; Yeye hatatenda sasa. Hilo si la siku hizi."

77 "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Hayo ndiyo Maandiko. Hilo ndilo tunaloamini kuwa ni Kweli. Hilo ndilo tunalokubali kuwa ni Kweli. Yeye ni yule yule katika kanuni.

Ni yeye yule katika nguvu. Ni yeye yule katika upendo. Ni yeye yule katika kila njia aliyokuwa wakati huo. Sasa Yeye amekuja pamoja na Kanisa, kama vile Mungu alivyomtuma na akaenda pamoja Naye. Kwa hiyo. . .

78 Na Mungu alimfufua. Kama Mungu hangekuwa pamoja Naye, kamwe asingalimfufua siku ya tatu. Kwa hiyo, Baba aliyemtuma, yuko pamoja Naye daima, alienda pamoja Naye kaburini, na akamfufua siku ya tatu.

79 Sasa, "Kama vile Mungu alivyonituma," alisema, "nami nawatuma. Nitakuwa pamoja nanyi, ndani yenu, daima, hata ukamilifu wa dahari." Wakati wa ufufuo, Pasaka yetu itakapokuja, Atakuwa pale sawasawa na vile Mungu alivyokuwa asubuhi ile ya Pasaka, akamfufua katika wafu!

80 Sasa, katika mfano wa jambo hilo, ameleta hili. Kabla ya kuweza kuwa na ufufuo, inabidi kuwe na kifo. Kwa maana, haina budi kuwa kitu kimoja, ndipo kiondoke na kirudi, ipate kuwa ni ufufuo. Inamaanisha "kurudishwa."

81 Na kabla mtu hajafufuliwa katika ufufuo pamoja na Kristo, hana budi kufa, kwa nafsi yake; kufa kabisa, kwa washirika wake wote wa kidunia; kufa, kwa tabia zake zote za kilimwengu; kufa kabisa, kwa kila kitu kiovu; na kufufuliwa, upya.

82 Kisha, kujifanya tupu kwa Roho Mtakatifu, kujifanya tupu Mwenyewe; na kuingia, hasa, kwa Roho Mtakatifu, kunapajaza mahali hapo. Ndipo anaweza kumwamini Mungu. Ndipo anaona kama Mungu anavyoona. Haoni kama walimu wanavyoona. Haoni kama washiriki wa kanisa wanavyoona. Anaona kama Mungu anavyoona. Ndipo anaona kwamba Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ndipo anaona ya kwamba nguvu za Mungu ni kuu tu leo kama zilivyokuwa wakati ule.

83 Na katika hali yake ya kale ya kimwili, unaweza kumwelimisha, kumng'arisha, kumfadhili masomo. Huenda yakamweka katika makanisa yaliyo bora zaidi, yampe mabenchi bora zaidi, washiriki bora zaidi. Kamwe hatakuwa tofauti mpaka kwanza afe, kisha afufuliwe upya tena. Naye Roho Mtakatifu aliyemwita na kumtuma yu pamoja naye, hata ukamilifu wa dahari. Amina. Loo, najua hilo linashangaza, lakini ni Kweli.

84 Basi, kama Kristo angalikuwa ndani yetu leo, angefanya mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani. Ikiwa Bwana Yesu amefufuka katika wafu leo, na anaishi miongoni mwetu, na alisema, "Mambo yale yale nifanyayo mimi, ninyi nanyi mtayafanya, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari." Basi, kuna njia moja tu ya kuthibitisha kama amefufuka katika wafu. Hiyo ni, wakati, Kanisa linaloamini hilo, Kristo atajitambulisha Mwenyewe kwa Kanisa hilo kwa nguvu Zake zile zile za kufufuka Kwake. Haina budi kuwa hivyo, marafiki.

85 Hili ama ni Neno la Mungu au ni Kitabu kidanganyacho. Hiyo ni kweli. Ama ni cha kweli au ni cha uongo. Na ama chote ni cha kweli au chote ni cha uongo. Kila Neno limevuviwa au hakuna hata moja la Hayo lililovuviwa. Ninataka kuliamini.

86 Paulo alisema, "Sikuja kwenu nikihubiri kwa maneno ya kushawishi na hekima ya wanadamu; kwa maana, ningalifanya hivyo, basi imani yenu ingejengwa juu ya hekima ya wanadamu. Lakini nilikuja kwenu, nikihubiri Injili ya Uweza wa Mungu, ufufuo wa Bwana Yesu, imani yenu ipate kuwa thabiti." Paulo kamwe hakuja na ujuzi fulani wa seminari, kung'arisha, na kuondoa na kuongeza.

87 Alisema, "Naja nikijua jambo moja tu; Kristo aliyesulubiwa. Nimekuja tu nikijua jambo moja, nikiwahubiria Nguvu za ufufuo, kwamba Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele." Na katika Wagalatia 1:8, alisema, "Malaika akihubiri jambo lingine lolote, na alaaniwe, kwenu." Hiyo ni kweli.

88 Sasa, Yeye alifufuka? Tuko hapa asubuhi ya leo kuuliza swali: Je, alifufuka?

89 Sasa, siku hizi, sherehe zinasemwa, kote ulimwenguni. Na wanazunguka na ninii kubwa...baadhi yao wakiwa na shanga za maombi, wakizikariri. Hiyo ni shauri yao. Wengine wanazunguka huku na huko, wakijivunia dhehebu kuu walilo nalo. Hiyo ni shauri yao. Wengine huweka misalaba mikubwa, na piano na vyombo, na majengo mazuri ya kanisa, na kusema, "Angalia yale tuliyo nayo! Walio bora zaidi wa mjini huja kwa kanisa letu." Hiyo ni sawa. Hiyo ni shauri yao.

90 Lakini sijui kitu ila kufufuka Kwake Bwana Yesu; liwe katika ghala, au zizini, popote liwezapo kuwa. Sitaki kujua kitu miongoni mwenu ila ufufuo. Sitaki kusikia jinsi mlivyo wazuri; kwa sababu wewe si mzuri, kwanza kabisa. Sisi si wazuri, kwanza kabisa. Jambo moja tu ninalotaka kujua, ni kufufuka kwake Bwana Yesu, ambako kumekuwa katika moyo wa mwanadamu. Basi, kama Kristo amekufa, naam, hajafa, bali amefufuka tena, basi Yeye yu pamoja nasi. Basi, mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani, anawajibika kuyafanya tena, kulingana na Neno Lake. Anawajibika. Na kitu hicho kinapofanywa tena juu ya nchi, kitu kile kile...

91 Sasa, alipokuwa hapa, hakudai kuwa mponyaji mkuu. Sivyo? Alisema Yeye hakuwa mponyaji. Alisema, "Sitendi lolote kwa nafsi Yangu. Sitendi lolote isipokuwa nimwone Baba akilitenda; na hilo atenda Mwana vile vile."

92 Alipitia kwenye birika la Bethesda, ambapo jamii kubwa ya watu ililala, viwete, vipofu, vilema, waliopindika, waliopooza, wakingojea kutibuliwa kwa maji. Naye huyu hapa Imanueli anakuja, huyu hapa Yesu anakuja, mavazi yaliyojaa wema.

93 Mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, siku chache kabla ya hapo, akaponywa kabisa. Alimgusa, kisha akakimbilia nje kusanyikoni akaketi chini, ama chochote kile. Yesu akasimama, akatazama huku na huku. Kasema, "Ni nani aliyenigusa?"

94 "Mbona," kasema, "angalia umati wa watu, Mwalimu! Kila mtu anakugusa."

95 Akasema, "Naam, lakini ni—nimekuwa dhaifu." Akasema, "Kitu fulani kimetendeka."

96 Naye akatazama pande zote, juu ya kusanyiko, mpaka akampata yule mwanamke. Akasema, "Sasa imani yako imekuponya kutokwa huko na damu." Mnaona? Imani yake ilimgusa.

97 Huyo alikuwa ni Yesu jana. Huyo ni Yesu leo. Huyo atakuwa Yesu milele. Maadamu kuna haja ya uponyaji, kutakuwa na Yesu wa kuponya. Maadamu kuna mwenye dhambi wa kuokoa, kutakuwa na Yesu wa kumwokoa. Huyo Ndiye.

98 Alipopitia katika umati huo mkubwa, alienda kule na kumponya mtu aliyekuwa amelala juu ya godoro, akaondoka na kumwacha. Mbona, wanafunzi wa Wayahudi, walisema, "Kumbe, tazama pale, tazama umati huo! Kwa nini hakwenda kule na kumponya *huyu*? Ningeamini." Na kadhalika namna hiyo, walimhoji. Walimwona mtu huyu akibeba kitanda chake, siku ya sabato.

99 Akasema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kufanya neno Mwenyewe."

100 Mnaona ambapo Yeye alitolea sifa zote? Roho yeyote wa kweli wa Mungu atafanya jambo lile lile. Atamsifu Mungu, kila wakati.

101 Kasema, "Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe. Lakini yale nimwonayo Baba anayatenda, hayo ndiyo mambo nitendayo. Baba anafanya jambo fulani, Naye ananionyesha, nami naenda kulifanya."

102 Kama huyo alikuwa ni Yesu wakati huo, haina budi kuwa ni Yesu leo. Hiyo ni kweli.

103 Alisimama katika kusanyiko la watu, na aliweza kutambua mawazo yao. Alijua shida yao. Alilitazama kusanyiko Lake, mara nyingi, na kusema, "Mbona mnafikiri hivi moyoni mwenu na kusema mambo tofauti?"

104 Mwanamke mmoja alimjia kisimani, wakati mmoja, Yeye akasema, "Nipe maji ninywe."

105 Akasema, "Kwa nini, si kawaida kwenu Wayahudi kuwaomba Wasamaria kitu kama hicho." Kasema, "Hatuna uhusiano."

106 Kasema, "Lakini kama ungejua ni Nani uliyekuwa ukiongea naye, ungeniomba Mimi maji unywe."

"Loo, sasa," akasema, "hiyo—hiyo inawezekanaje?"

Naye akasema, "Nenda kamwite mumeo."

Akasema, "Sina mume."

107 Kasema, "Hiyo ni kweli. Unao watano." Kisha akasema, "Yule unayeishi naye sasa siye mume wako."

108 Akasema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii." Akasema, "Sasa, ninajua hiyo itakuwa ndiyo ishara ya Masihi." Akasema, "Ninajua ya kwamba ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya, lakini u Nani Wewe?"

Akasema, "Mimi ninayesema nawe, Ndiye."

109 Haya basi. Hiyo ilikuwa nini? Ishara ya Masihi. Amina. Angalieni. Na, mle ndani, hawakuielewa. Hawakuelewa hiyo ilimaanisha nini. Iliyapofusha macho yao. Miujiza Yake na kadhalika iliyapofusha macho yao.

110 Na ndivyo ilivyo siku hizi. Mambo yale yale yatayapofusha macho ya nia ya kimwili, kwa sababu haiwezi kuelewa mambo ya Mungu. Ni kinyume na Mungu. Ni adui wa Mungu. Akili ya mwanadamu ni adui wa Mungu. Huna budi kutoka katika nia yako mwenyewe ya kibinadamu, na kuzaliwa upya, kwa Roho Mtakatifu, na kuwa na nia ya Mungu ndani yako. Ndipo unaweza kuamini mambo hayo. Kisha yanakuwa halisi. Amina.

111 Sasa angalieni basi, alipokuwa hapa, mambo aliyofanya. Wakati akiondoka, aliliambia Kanisa Lake, baada ya kufufuka Kwake, akasema, "Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari." Macho yao yakafumbuliwa. Wakafahamu.

112 Petro na hao wengine, kabla ya hapo; baada ya kuwa rafiki Yake wa karibu, alitembea pamoja Naye, akazungumza Naye. Ndipo Petro akasema, "Loo, nimevunjika moyo sana! Baada ya kifo hiki kule juu, nao wakamzika. Ni—nimevunjika moyo sana. Naamini nitaenda tu kuvua samaki."

113 Basi wanafunzi walikuwa wamesimama hapo karibu, nao wakasema, "Tutaenda nawe tu." Kwa hiyo, hao, wakachukua wavu wao. Wamevunjika moyo! Waaminio, wakati mmoja, theolojia ya akili. Waliamini, wakati mmoja, kimwili. Lakini, jaribio dogo lilipotokea, yote yalisambaratika.

114 Sasa, hapa, sikusudii kuwadhuru, bali nataka kuwarekebisha. Mnaona? Hiyo inaonyesha tu wakati mtu ana imani ya kiakili tu, kwa kusema, "Naam, hilo ni Neno la Mungu. Naam, naamini Mungu alimfufua Yesu siku ya leo." Kisha, hiyo, hiyo ndiyo tu uliyo nayo. Kuvunjwa moyo kidogo kwa kwanza kukitokea kanisani mwenu, unaondoka, unaenda zako. Mnaona? Unaweza kuwa rafiki Yake, lakini humjui katika Nguvu za kufufuka Kwake.

115 Hakuna wakati mmoja, baada ya Pentekoste, ambapo mhubiri huyo, Petro, aliwahi kusema jambo kama hilo.

Walipokuwa tayari kumwua, walikuwa wanaenda kumtundika msalabani. Akasema, “Hata sistahili kufa namna hiyo. Geuzeni miguu yangu juu; kichwa changu chini. Kwa sababu, Bwana wangu alikufa namna hiyo, huku kichwa Chake kikiwa juu.” Naam, kamwe, kamwe. Mnaona? Alikuwa pamoja na Kristo wakati ule, lakini wakati huo Kristo alikuwa ndani ya Petro. Petro alikuwa anaongoza wakati ule, kisha, baada ya Roho Mtakatifu kuja, ndipo Roho Mtakatifu akawa anaongoza. Petro alikuwa nyuma, kisha Roho Mtakatifu akamwongoza.

116 Sasa ikiwa unaninii tu. . . Ikiwa una hoja nzuri, utaketi chini na kujaribu kuihoji Biblia, kuhoji, “Angewezaje kufufuka katika wafu? Miujiza hii na kadhalika ingewezaje kutukia siku hizi, katika nyanja hizi kuu za ustaarabu, sayansi tunazoishi?” Ukijaribu kuhoji hilo, unaenda tu mbali zaidi na Mungu, wakati wote. Hutamjua kamwe kwa hoja. Mungu hajulikani kwa hoja.

117 Mungu anajulikana kwa imani. Unaikubali. Unaiamini. Huwezi kufanya hivyo mpaka jambo fulani litendeke ndani yako, ndipo Roho Mtakatifu anaingia nawe una nia ya Kristo.

118 Angalieni. Wao, usiku kucha walivua samaki, wala hawakupata samaki. Inavunja moyo sana! Kesho yake asubuhi, mapema, kwenye ibada ya mapambazuko, walitazama ng’ambo ya ukingo, na hapo alisimama Yesu. Lakini hawakumtambua. Hiyo ndiyo sehemu ya kusikitisha. Hawakumtambua.

119 Usiku mmoja, maskini ile mashua ya kale ilikuwa karibu kuzama, baharini, kwenye dhoruba. Naye huyu hapa Bwana mwema akiwakaribia. Wakasema, “Loo, ondoka. Ni mzimu. Ni mzuka. Hatutaki uhusiano wowote Nao.” Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, kilikuwa karibu nao, nao walikuwa wanakiogopa.

120 Na hebu niseme hivi kwenu ninyi watu, leo, ambao hamjapata kumpokea Roho Mtakatifu. Ninatambua, katika milki za kanisa, tuna dhihaka nyingi. Tuna wengi wanaojifanya kuwa na Roho Mtakatifu, wakati hawana. Hiyo ni kweli. Vivyo hivyo nanyi mnao katika milki zenu huko, pia, wanaodai kuwa washiriki wa kanisa, nao sio. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, palipo na mema, pana mabaya. Kumbukeni hilo. Palipo na hasi, pana chanya. Palipo na dola bandia, pana iliyo halisi. Na palipo na mtu anayedhihaki na kujifanya kuwa na Roho Mtakatifu, pana Roho Mtakatifu wa kweli. Kumbukeni hilo.

121 Na Kitu kile kile kitakachokusaidia; Kitu kile kile ambacho kitakukomboa; Kitu kitakachokutoa katika gereza lako la tabia, kitakachokutoa katika vyumba vyako vya gereza la hofu na fadhaa; Kitu ambacho kitakuondoa kwenye kansa na kukufanya kiumbe hai tena; kile Kitu kitakachokuinua katika siku za mwisho; kinasimama papo hapo karibu nawe, nawe unakiogopa. Usiogope. Ni Yeye.

122 "Ni Mimi," alisema. "Msiogope. Ni Mimi." Lakini walikuwa wanakiogopa; kuogopa kuamini Neno Lake kulihusu. Alisema, "Ni . . . Msiogope. Ni Mimi."

123 Yesu akawauliza kama walikuwa na samaki yeyote. Wakasema, "La." Kasema, "Tumefanya kazi usiku kucha." Nao wakafika ufuoni wakakuta samaki wamepikwa na kuwekwa tayari kwa ajili yao. Wakajua, kwa mwujiza huo, ilikuwa ni Yeye.

124 Wawili zaidi, walipokuwa wakienda zao mbio Emau. Sikilizeni kwa makini sasa tunapofunga. Wakienda zao Emau siku moja, baada ya ufufuo, kulikuwa na watu wawili; mmoja, Kleopa, na rafiki yake. Asubuhi nzuri ya sabato kama hii, Pasaka ya kwanza nzuri.

Kwa makini sasa, liangalieni Neno. Iweni tayari.

125 Nao walipokuwa wakiiadhimisha Pasaka ya kwanza, huku wamevunjika moyo, wamevunjika moyo kwa sababu sikitiko lilikuwa limeingia.

126 Huenda kukawa na wanaume na wanawake hapa, leo, wanaoadhimisha Pasaka hii kwa sababu ya sikitiko, jambo fulani lilifanyika. Lakini, kumbukeni tu, Bwana Yesu amefufuka kutoka kaburini leo. Anaishi miongoni mwa watu.

127 Mara nyingi, nilipokuwa shuleni, tulisoma botania. Sikuzote nimesoma botania. Botania, kwangu mimi, zaidi sana, sio maisha ya mimea; kuangalia jinsi mmea unavyokuzwa, na jinsi jua linavyokuja, na kadhalika. Botania, kwangu mimi, ni Yeye Yule aliyeiumba, ni Muumba aliyeufanya mmea ukue. Loo, jinsi maua hayo ya Pasaka yanavyopendeza! Yaangalie. Loo, jamani! Hayo maua mazuri ambayo yanakaa huku, hakuna mtu ambaye angeweza kuutazama uso wa moja na kusema hakuna Mungu, na awe na akili timamu.

128 Nao hawa hapo, wamevunjika mioyo, wanarudi nyumbani. "Vema, tulianza. Tulidhani itakuwa sawa, lakini inatubidi kurudi nyumbani sasa, basi, wakienda zao kurudi Emau." Basi walipokuwa wakitembea, wamesikitika, wao . . .

129 Mazungumzo yalikuwa sawa. Walikuwa wakizungumza juu Yake. Hapo ndipo alipotokea.

130 Na hiyo ndiyo sababu Yeye haonekani kwa wengi wetu siku hizi, mazungumzo yetu ni kuzungumzia mengine yote isipokuwa Kristo. Daima tunazungumza kuhusu wakati tutakapomaliza kazi, au tutakayofanya hapa. Acha mazungumzo yenu yawe juu ya Kristo. Hapo ndipo anapotokea, ni hapo mnapozungumza juu Yake. Iweni mkizungumza juu Yake.

131 Nao walikuwa wakienda zao, wakiongea habari Zake. Hata hivyo, walimpenda, hawakujua kwamba alikuwa amefufuka katika wafu.

132 Na watu wengi, siku hizi, ambao kweli wanampenda Bwana Yesu, huko nje katika makanisa haya makuu kote ulimwenguni, wanampenda Bwana, lakini kweli hawajui kwamba amefufuka katika wafu.

133 Angalieni. Alipokuwa akienda zake, Mgeni mmoja alitokea kichakani na kuwasalimia, “Habari za asubuhi,” labda. Na wao, huku wamehuzunika kabisa, wamevunjika moyo, wakisema, “Loo, nilimpenda. Nilimwona akisimama kando ya kaburi la Lazaro, wakati mtu aliyekuwa amekufa siku nne, na kusema, ‘Lazaro, njoo huku.’ Loo, Mtu huyo angewezaje kushindwa? Angewezaje kutuaibisha namna hii? Na sasa tunasimama katika aibu na fedheha? Tunarudi nyumbani kuanzisha uvuvi wetu na useremala tena.” Mnaona?

134 Je, huyo si ni Mkristo wa kisasa tu siku hizi? Loo, hebu uponyaji na utendeke, nao wanapiga kelele za ushindi. Hebu Nguvu za Roho Mtakatifu zishuke, nao wanapiga kelele za ushindi. Na wale ambao kwa kweli wamejazwa na Roho Mtakatifu, wanabaki hivyo katika safari ya maisha.

135 Lakini mtu ambaye angali anatembea na nia ya kimwili, hebu hali ya kuvunjwa moyo kidogo itokee, kitu fulani kiende mrama, ndipo wanaondoka, wakisema, “Vema, nilifikiri ilikuwa sawa, lakini, loo, jamani, hebu liangalieni sasa. Nilifikiri kwamba maskini kanisa hilo halingeshindwa kamwe. Nilifikiri mtu huyu . . . ” Umeweka mawazo yako kwenye jambo lisilostahili. Unaona? Weka mawazo yako juu yake Yeye asiyeweza kushindwa. Mazungumzo yako yasiwe kuhusu kanisa lako, bali kuhusu Bwana wako. Huyo Ndiye. Si kuhusu jirani yako, bali juu ya Bwana wako. Maongezi yenu yawe juu Yake.

136 Basi, walipokuwa wakisafiri, wakizungumza; kwa ghafla, Mtu, Mtu wa kawaida tu . . .

137 Hakuwa mwandishi mkuu. Hakuwa na elimu. Hakuwa amesoma. Kadiri tujuavyo, Yeye hakuwahi kwenda shuleni hata siku moja maishani Mwake, lakini alikuwa na hekima kupita mwanadamu yeyote aliyepata kuishi. Mafarisayo walipoona hekima Yake, walisema, “Alisomea shule gani? Alitoka wapi? Unapata wapi Maneno haya? Anafanyaje jambo *hili*? Sisi . . . kamwe hakupitia seminari zetu. Haongei kama mmoja wa watu wetu. Maneno haya yanatoka wapi?” Na hapo walichukizwa kwa sababu Yeye hakuwa mfuasi wa makundi yao. Hakujihusisha Mwenyewe nao. Alionekana wazi wazi, dhahiri, kwa maana Yeye alikuwa ni Mungu.

138 Hapo alisimama, na kujitambulisha Mwenyewe. Akasema “Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi nizifanyazo. Zinashuhudia kwamba Baba alinituma.” Alisema, “Na elimu Yangu . . . ” Kwa maneno mengine, namna hii, “Ikiwa elimu Yangu haikidhi matamanio yenu, kama digrii Yangu . . . Ambayo, sina. Lakini, digrii Yangu, diploma Yangu, haitokani na

seminari zenu. Diploma Yangu ni kazi nizifanyazo, ambazo Baba alinituma. Ndizo diploma Yangu." Hiyo ndiyo diploma bora kuliko zote niijuayo. Mungu, tupe diploma hizo zaidi! "Kazi nizifanyazo Mimi ni thibitisho kwamba Baba alinituma. Ikiwa hiyo haitoshi, ziaminini basi badala Yangu."

139 Sasa mwangalieni Yeye. Loo, ninampenda! Ninapomwona akitembea pale, Naye alisema, "Mbona mna huzuni hivi? Ni nini kinachowafanya mjisikie hivi? Ni siku ya kupendeza jinsi gani! Angalieni jinsi kila kitu kinavyoonekana!"

140 Akasema, "Naam," kasema, "Najua, lakini tuliamini . . ." Kasema, "Je, wewe ni mgeni tu hapa? Mbona," kasema, "hujui ya kwamba, Yesu wa Nazareti, Mtu aliyethibitishwa na Mungu, kwa ishara kuu na kadhalika? Tulimfuata kwa miaka mitatu na nusu. Na—naye Pilato akamsulubisha. Nao wakamzika, wakamlaza kaburini. Mbona," wakasema, "tulikuwa na matumaini kwamba angekuwa mfalme, kiongozi mkuu. Na sasa Yeye amelala pale, yumo kaburini, amepakwa dawa asioze, na amelazwa kaburini."

"Mbona," akasema, "kwani hamyajui Maandiko?"

141 Loo, napenda hilo! Alifanya nini? Alienda moja kwa moja kwenye Maandiko, kuthibitisha hoja Zake. Na Roho yeyote wa kweli wa Mungu ataenda moja kwa moja kwenye Maandiko.

142 Alifanya nini? Alirudi katika Agano la Kale, Vitabu vya Musa, na kuanza kuzungumza juu ya Musa na juu ya watu wengine, jinsi ambavyo walisema ya kwamba Yesu angekuja, jinsi angeteseka na yale ambayo angefanya. Akasema, "Je, hamjui hili, Maandiko, Neno?" Kasema, "Je, hamjui ya kwamba Neno hilo lililokuwako huko nyuma limefanywa hai? Hamjui kwamba Kristo alipaswa kufufuka katika wafu? Na kuna . . . "

143 "La, hatukujua hilo." Watu wema, waliompenda, lakini hawakujua kwamba alikuwa amefufuka katika wafu.

144 Ndivyo ilivyo siku hizi, jambo lile lile leo, hasa, ndugu, dada. Loo, Mungu na auamshe utu wako wa ndani kabisa! Watu hawaelewi kwamba amefufuka katika wafu. Yeye hajafa. Yu hai.

145 Naye akatoka nje, akiwa amejificha. Alionekana kwao katika umbo la Mwanadamu.

146 Anaweza kukutokea katika umbo la jirani yako. Anaweza kukutokea katika umbo la m—mhudumu, au mama yako. Kristo hukutokea katika watu. Basi, mtendee kila mtu haki, kuwa mwenye fadhili, kuwa jirani mwema, kuwa na upendo. Kristo yuko ndani ya huyo mtu. "Kristo ndani yako, tumaini la Utukufu." Na unapoendelea, na watu wanakutokea, mtu mwenye fadhili anaanza kuzungumza nawe, wasikilize. Hujui, inaweza kuwa ni Yesu akiongea nawe. Unaona, anatokea. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Na mnapowafanyia hawa, mnanifanyia Mimi."

147 Loo, unapoanza kuliangalia hivyo, mapokeo ya kale yanatoweka. Unaona? Haliwi mfano wa maneno, na tangazo la maneno mengi yaliyowekwa pamoja. Inakuwa ukweli hai kwamba Kristo yu ndani yetu sasa. Roho Mtakatifu akienda huku na huku, kupitia kila mwanadamu, akienea mioyoni, akichunguza, akihukumu maisha magofu mle ndani. Na unapokiri jambo hilo, Yeye analiweka mbele za Mungu, nayo Damu inalisafisha. Amina.

148 Ndipo, walipokuwa wakiendelea mbele, sasa tazama, ilikuwa inaelekea wakati wa jioni. Loo, ninapenda hili sana!

149 Laiti tungekuwa na zaidi kidogo. . . Loo, jamani! Sikujua nilichukua muda mrefu hivyo.

150 Tazama. Ilikuwa inaelekea jioni. Nitafunga. Je, mliona? Sasa sikilizeni kwa makini. Ilikuwa inaelekea jioni. Naye akafanya kana kwamba angeendelea mbele na kuwaacha, bali wao wakamshawishi aingie.

151 Nashangaa tungefanya ushawishi kiasi gani leo? Nashangaa unafanya kiasi gani sasa hivi? "Ee Bwana, Wewe uliyefufuka, niruhusu nikushawishi uje moyoni mwangu. Ingia pamoja nami. Ninataka kukuamini. Nimeishi maisha ya Mkristo nusu, kwa hiyo mimi. . . kwa kuamini tu imani ya maarifa, na kadhalika, imani ya kiakili. Lakini ninataka kukujua katika Nguvu za kufufuka Kwako, kwa maana huu ndio wakati pekee ambao itanibidi kufanya maandalizi. Ninataka kukujua Wewe nitakapolaza kichwa changu chini nisiamke tena. Ninataka kukujua katika Nguvu za kufufuka Kwako. Sitaki kubahatisha tu juu yake. Nataka kukujua Wewe. Je, utaingia tu na kukaa nami? Siku imeenda sana."

152 Angalieni, walipoingia ndani, wakafunga milango, Yeye angeweza kuzungumza nao basi. Ni tofauti ya jinsi gani aliyofanya kutoka kwa watu hawa! Hao waliosimama ukingoni hawakumjua; walikuwa wamekaa Naye muda mrefu. Lakini wakati, Kristo, mara alipoingia ndani. . .

153 Sio Kristo akiwa *nje*, akilisoma, akisema, "Naam, hiyo ni kweli." Bali Kristo akiwa *ndani*, akisema, "Hiyo ni kweli." Mnaona tofauti? Kristo akiwa ndani! Naye akasema. . .

154 Mara akiwa ndani, mlango umefungwa. Ndipo akajitambulisha kwao, kwa jinsi alivyofanya jambo fulani. Aliutwaa mkate akaumega.

155 Nao wakaangalia, wakasema, "Kuna Mtu mmoja tu duniani angeweza kufanya hivyo, na huyo ni Yeye." Jinsi tu alivyofanya jambo fulani! Si jinsi alivyopanga mahubiri Yake; maana walikuwa na wanatheolojia chungu nzima wakifanya hivyo. Si jinsi alivyovalia; kwa mtindo wa Hollywood, ingekuwa leo. Si hivyo. Lakini, jinsi alivyofanya jambo fulani, walijua ya kwamba

hiyo ilikuwa ndiyo njia Yake ya kufanya jambo hilo. Ndipo macho yao yakafumbuliwa. Wakamtambua basi.

156 Hawakumtambua kwa siku chache. . .au wanafunzi ambao hawakumwona hivyo. Hawakuwahi kufungiwa ndani pamoja Naye. Hawakumtambua walipomwona. Lakini wale ambao waliwahi kufungiwa ndani, walijua alikuwa ni Bwana wao.

157 Nami nataka muone jambo fulani. Kwa makini sasa kabla ya kufunga, kufunga. Asubuhi iyo hiyo na mapema, Mariamu Magdalene na Martha walipokuwa kaburini, kwanza. Sikilizeni. Kwanza, mapema asubuhi hiyo, Kristo alijionyesha Mwenyewe wazi miongoni mwa walioamka mapema. Wala hakujionyesha tena, siku nzima, mpaka wakati wa jioni. Ndipo akajitambulisha Mwenyewe tena, kwa maana Yeye alikuwa Alfa na Omega.

Itakuwa Nuru wakati wa jioni,
Njia ya Utukufu bila shaka mtaipata.

158 Kristo alipojitambulisha siku za mwanzoni pamoja na mitume, kwenye ufufuo, kwa ishara na maajabu ambayo Petro, Yakobo, Yohana, na hao wengine walifanya, Yeye alijitambulisha kwa watu, vipi? Katika Nguvu za kufufuka Kwake, sikilizeni, kwa ishara na maajabu na miujiza aliyofanya. Je, hiyo ni kweli? Alijitambulisha Mwenyewe.

159 Sasa tumepitia siku nzuri sana. Hiyo siku imepita; kupitia kwa walimu mashuhuri, Mtakatifu Augustino; tukashuka hadi kwa Martin Luther, John Wesley, Calvin, Knox, hao wote; tukashuka kwenye wakati wa—wa Methodisti, wakati wa Baptisti, wakati wa Nazarayo, wakati wa Pilgrim Holiness, wakati wa Kipentekoste. Nyakati hizi zote zimepita. Jua linashuka.

160 Yeye alisema, "Itakuwa Nuru wakati wa jioni. Kutakuwako na siku," alisema nabii, "ambayo haitakuwa mchana, wala haitakuwa usiku. Itakuwa tu kitu kama ukungu."

161 Na, leo hii, hivyo ndivyo ulimwengu umesafiri, tangu ile asubuhi ya kwanza ya kufufuka kwa Bwana Yesu, na wakati ule wa kwanza wa kanisa kule nyuma, katika—katika Wakati wa Kanisa la Efeso. Wakati wa kwanza kabisa kule, Mungu alijitambulisha kwa ishara na maajabu na miujiza. Ulififia katika wale waanzilishi wa mwanzoni. Ukashuka kupitia kanisa Katoliki, hadi kwenye yale matengenezo, kupitia hapa. Wamekuwa na Nuru ya kutosha kuamini ya kwamba Yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Wamekuwa na Nuru ya kutosha kumkubali kama Mwokozi binafsi, na imeshuka. Lakini mawingu, yale mawingu ya giza, walimu waliowafunga watu, wakisema, "Siku za miujiza zimepita. Mambo haya yote yamepita, miaka mingi iliyopita." Imekuwa siku yenye giza. Sio giza kwa jumla; wangeweza kuona jinsi ya kutembea, lakini si vizuri sana.

162 Lakini, ndugu, Mungu aliahidi wakati jua lilipokuwa linatua kwenye ulimwengu wa Magharibi, kwamba itakuwa Nuru tena, bila shaka kabisa.

163 Biblia hii ni Kitabu cha mashariki. Imeandikwa katika desturi za kimashariki. Imeandikwa katika tabi-. . .lugha, mashariki. Jua huchomoza mashariki, likatua magharibi. Na katika watu wa mashariki, walikuwa na siku yao ya kujiliwa kwenye ufufuo wa kwanza. Nalo jua limepitia katika nyakati. Nao ustaarabu ulianza kutoka mashariki, kwenda magharibi. Na kabla tu jua kutua hapa kwenye upeo huu wa magharibi, itakuwa Nuru tena. Bwana Yesu yeye yule aliyefufuka atakuja katika Nguvu Zake zile zile. Kama vile alivyojitambulisha Mwenyewe kwa Mariamu Magdalene na hao wengine, hapo mwanzoni, Anajitambulisha Mwenyewe katika Nguvu za kufufuka Kwake, kwenye wakati wa mwisho. Wapi? Katika wakati wa mwisho.

164 Alisema, "Ingia ndani. Kumekuchwa. Mchana umekwisha. Inaelekea jioni. Hivi hutaingia?" Nao wakamwingiza ndani.

165 Basi alipoingia ndani, aliyafumbua macho yao. Alifanya jambo fulani. Wakasema, "Ni Yeye pekee angeweza kufanya jambo hilo."

Angalia jinsi walivyokuwa. Walisafiri siku nzima.

166 Hapo ndipo wamishenari wameshindwa. Tumefulia kwenye mbao za kufulia, kuwasaidia wamishenari waliokwenda kule, kusambaza vitini. Tumetuma watu huko kufundisha theolojia. Na kuna Mudha, Budha, Islamu, Mabaniani, nanii. . .Dini zote mbalimbali za ulimwengu ziko mle ndani na theolojia ile ile yao ambayo inaweza kutoa kitu kile kile Ukristo unachoweza, kwa njia ya saikolojia. Hiyo ni kweli.

167 Na ulimwengu, ni theluthi moja tu yao, katika asubuhi hii ya Pasaka, wanaojua ama wamewahi kusikia kuhusu Yesu. Theluthi mbili za ulimwengu ziko katika ukomunisti na gizani. Theluthi mbili za ulimwengu hawajawahi kusikia kuhusu Yesu wala ufufuo.

168 Lakini, ndugu, tukio la Emau lilipomjia Kleopa, macho yao yalipofumbuliwa, nao wakatambua walikuwa ni nani! Na, kwa muda wa dakika chache, wakasafiri katika ushoroba wa wakati, wakarudi Yerusalemu, wenye miguu myepesi, wachangamfu, wakiwaambia watu. "Tunajua Bwana wetu amefufuka katika wafu, kwa kuwa tumemwona na tunajua kwamba Yeye ni halisi."

169 Jambo ni kwamba, ni siku za mwisho. Mungu atawainua wakiwa na jumbe, pamoja na nguvu, pamoja na ukombozi, pamoja na nguvu za Injili, kuthibitisha ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

170 Najua linasikika la kusisimua. Si ajabu! Tunaishi katika wakati wa kusisimua. Naam, ndivyo ilivyo. Tunaishi katika siku za mwisho. Wakati, Mungu, kupitia kwa kila nabii mtakatifu, kupitia Agano lote la Kale, kupitia Agano Jipya, ametabiri, ya kwamba katika wakati wa mwisho mambo yale yale yaliyotukia hapo mwanzo yatatukia katika wakati wa mwisho, na kwa kuwa giza lingeondoka, na Nuru ya Injili ingeangaza katika ushoroba wa dunia, mara nyingine tena, kabla ya Kuja Kwake Bwana Yesu.

171 Amefufuka katika wafu. Yeye ni yeye yule jana, leo, na atakuwa milele. Yesu Kristo alifufuka katika wafu na anaishi kati yetu. Nina furaha sana kwa hilo. Moyo wangu umesisimkwa kupita maneno. Wakati, haitubidi kubahatisha juu yake. Ni Ukweli.

172 Mungu akubariki, rafiki. Kama hujui hilo . . . Usimwangalie yeye anayeuleta Ujumbe huu, bali kizingatie kile Ujumbe huu unachomaanisha. Mnaona? Ni kwako wewe uliye nje ya Kristo. Kama humjui katika Nguvu za Kufufuka Kwake, kama unaninii tu . . . Usichukue dhana za kiakili juu yake. Usizungumze kuhusu theolojia yako au imani yako ya kiakili; kama jambo fulani halijashuhudia moyoni mwako, na moyo wako umetupwa nje ukawa kaburi tupu (haleluya) kwa mambo ya kale yaliyokufa ya ulimwengu, naye Kristo amefufuka upya moyoni mwako.

173 Ee Mungu, asubuhi ya leo, fingirisha na kuondolea mbali jiwe la shaka. Liondolee mbali.

174 Naye na ainuke leo moyoni mwako, na kukufanya kiumbe kipya. Nami ninaamini ya kwamba atajitokeza jukwaani, katika dakika chache, na atafanya mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani.

Na tuombe, huku tumeinamisha vichwa vyetu.

175 Baba yetu wa Mbinguni, kunachelewa. Muda umeenda sana. Lakini, ilikuwa kwenye saa iliyotumika wakati ulipotokea. Tunakushukuru kwa ajili ya Maneno Yako ya Kiungu. Tunakushukuru kwa ajili ya Injili hii tunayohubiri na kuamini. Tunakushukuru kwa ajili ya Injili hii ambayo umeithibitisha kuwa ni Kweli.

176 Na sasa, Bwana Yesu, sema na nafsi zilizopotea. Watu wengi hapa, Bwana, wanaokupenda, lakini kwa kweli hawajawahi kukukubali. Unatembea nao kila siku. Wewe Ndiwe uliyewazuia kuuawa wakati huo kwenye ile ajali. Wewe Ndiwe uliyeizuia dhoruba isipeperushe nyumba siku ile, usiku ule. Wewe Ndiwe uliyewajia wakati wa taabu. Wewe Ndiwe uliyewapa kazi wakati hawakuwa na yoyote. Wewe Ndiwe uliyeifariji mioyo yao wakati wapendwa wao walipoingia kaburini. Umetembea pamoja nao, lakini, hata hivyo, hawakujui Wewe.

177 Mungu, jalia leo kwamba kila mtu hapa, aliye nje ya Kristo, atafanya kama Kleopa na rafiki yake walivyofanya, “Njoo

ukae nasi. Siku ya maisha yangu imetumika sana. Ingia sasa uitengeneze njia Yako."

178 Na wakati tumeinamisha vichwa vyetu, popote ndani au nje, kuna mtu hapa angesema, kwa mkono ulioinuliwa kwa Mungu, si kwa ndugu yako, bali kwa Mungu, "Loo, jambo fulani linatukia moyoni mwangu, asubuhi ya leo. Na—najua ya kwamba kuna jambo linalofanyika moyoni mwangu. Kamwe si—sitawahi kuwa vivyo hivyo. Ninaamini jambo fulani limetendeka tangu nilipokuja katika jengo hili asubuhi ya leo. Sasa ninamkubali Kristo moyoni mwangu, kama Mwokozi wangu. Ninataka kumwinulia Mungu mikono yangu, na kusema, 'Mungu, mimi hapa. Hili ndilo lote ninaloweza kufanya ni kuinua mkono wangu, kukwambia ninakuamini.'"

179 Hivi utainua mkono wako? Mungu akubariki, bwana. Hiyo ni sawa. Mtu mwingine yeyote, utainua mkono wako, useme, "Sasa namkubali"? Mungu akubariki, mama. Hilo ni sawa. Mtu mwingine?

180 Unapoinua mkono wako, Mungu aliahidi kukupa Uzima wa milele. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa milele. Hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

181 Je, utainua mkono wako sasa, useme, "Bwana, ninaamini"? Hakuna anayeangalia; mimi na Bwana Yesu tu, tafadhali. Inua tu mkono wako, useme, "Sasa ninamkubali kama Mwokozi wangu." Je, unaweza kuinua . . . Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe. Loo, hilo ni sawa, mikono kadhaa tu. Mungu akubariki. Hilo ni sawa.

182 Linakufanyia nini? Linakupa Uzima. Uliinua mkono wako kwa Bwana, ukasema, "Ninaliamini."

183 Yesu alisema, "Aaminiye hatahukumiwa kamwe; amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Sasa hivi unao Uzima wa milele. Je, hulifurahii?

184 Je, kuna mwingine kabla hatujaomba, mmoja zaidi ambaye angesema, "Ndugu Branham, asubuhi hii ya Pasaka, mimi sasa, kabla hata sijaona ishara dhahiri za kuonekana kwa Kristo, kama atafanya hivyo, sasa ninamkubali kabla sijaona chochote. Sitakuwa kama Tomaso, kungoja mpaka nitakapomwona na kumgusa, na kadhalika, na kisha kusema. Nitamkubali sasa hivi."

185 Alisema, "Thawabu yao ni kubwa zaidi jinsi gani, ambao hawajaona bado, wala kugusa, wala chochote, bali wameamini!"

186 Je, kuna mwingine unayeweza kuinua mkono wako, ndani au nje? Mungu akubariki, na wewe, na wewe. Wewe, dada, Mungu akubariki. Wewe, dada, Mungu akubariki.

Vema, tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu.

187 Baba yetu wa Mbinguni, Wewe umesema, "Lihubiri Neno. Uwe tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa. Karipia, kemea kwa uvumilivu wote na mafundisho." Usihubiri Injili nyingine isipokuwa ile tuliyokabidhiwa. Kristo alikufa, akafufuka tena siku ya tatu, kulingana na Maandiko; sasa ameketi katika mahali pa Mbinguni, Mbele za Ukuu wa Mungu, akifanya maombezi tunapoungama. Nalo Hili ni Neno Lake, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa milele."

188 Na, leo, katika ujumbe huu ulioharakishwa, uliotawanyika, wengi wameinua mikono yao. Umewaona. Ungewezaje hata Wewe kukosa kuwaona, wakati unajua kila shomoro anayeanguka barabarani! Unajua. Mungu mkuu mwenye uwezo wote, unaona kila kitu, unajua kila kitu, na unaweza kufanya kila kitu. Sasa, kulingana na Neno Lako, umewaokoa hawa kutoka dhambini, nasi tunakushukuru kwa ajili yake, Baba. Maisha yao na yawe marefu, yenye furaha. Na wakutumikie Wewe siku zote za maisha yao.

189 Wakija, usiku wa leo, ikiwa hawajawahi kuzamishwa, jalia waje wakabatizwe, wakiliitia Jina la Bwana, na wajazwe na Roho Mtakatifu usiku uu huu. Tujalie, Mungu mpendwa. Tunaomba katika Jina la Kristo.

190 Sasa, Baba, tunaingia kwenye ibada. Najua Neno Lako haliwezi kushindwa. Lilisema, kwamba, katika mji wetu wenyewe, "Mtumishi, katika mji wake kati ya watu." Lakini, mara mbili, Bwana, umeliruhusu litendeke, katika miaka hii kumi. Je, hutatujalia tena leo? Ni Pasaka, na nia zetu zote ni safi juu ya mawazo ya Pasaka, juu ya ufufuo. Ni safi, upya, juu ya Injili, asubuhi ya leo, kutokana na kuisikia ikihubiriwa hapa mara mbili. Nasi tunataka kukuona Wewe, Bwana. Nami nimewaambia watu ya kwamba Wewe uko hapa. Ulisema ulikuwapo. Ulikuwa kila mahali, sikuzote. Hivi hutakuja sasa na kuchukua hivi vyombo, ingawa ni duni, Bwana, vya maskini mtumishi Wako? Fanya kazi kupitia sisi, leo, ili kwamba wanaume na mwanamke wanaoketi hapa, na wale ambao wamekukubali sasa hivi, wataona waliyoyafanya; kwamba si kitu cha uwongo; Ni Bwana Yesu. Ee Mungu, tujalie. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

191 Loo, jamani! Je, mnajisikia vizuri? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ninajisikia hivyo tu, ingawa nimechoka na nimedhoofika. Jinsi tu Neno lilivyo tukufu!

Sasa, marafiki, kuhubiri kwote ambako ningeweza kufanya . . .

192 Ki—kidogo mimi . . . Leo, nimekuwa nikihubiri mara mbili. Sina budi kuharakisha, kesho, kuendesha gari. Sina budi kuondoka asubuhi na mapema kuelekea Tacoma, Washington,

na kwenda Canada. Nao walitaka nipande ndege, nipate kuwa kwenye ibada kesho, lakini huenda nitaenda kwa gari.

193 Kwa hiyo sasa angalieni, sasa, mahubiri yote ningeweza kufanya; jambo moja Kristo angeweza kufanya, na liwe na thamani ya mambo yote ambayo ningeweza kusema katika miaka elfu moja, kwenu, kama mngeweza kuishi kuliona.

194 Sasa nataka kuwauliza jambo fulani, nami ninawatakeni muwe na kicho kabisa. Sasa, wengi wenu wanasimama. Najua mumechoka, lakini tupeni tu dakika chache. Sasa, ninachukua hii. . .

195 Eleweni, sisemi itakuwa. Mimi, kwa imani, kwamba nimemwomba Mungu kufanya hivyo. Nami ninamwomba sasa ya kwamba angeleta mkutano hapa, kama tu anavyofanya hudumani, kwamba watu hapa Jeffersonville wangejua ya kwamba Yesu alifufuka katika wafu. Sasa, tumekuwa nayo mara mbili.

196 Sijui ni lini nitarudi baada ya leo, maskanini, tena. Nalipenda maskini kanisa hili la kale. Sio zuri sana, kwa wageni waliopo. Papa hapa kuna alama za vidole vyangu, bado, kwenye mimbara hii, kwa miaka kumi na miwili ya kuhubiri hapa. Nina miaka ishirini na mitatu katika Injili sasa.

197 Loo, nimekuja mbali sana hata kutazama nyuma! Loo, nimeona mengi sana! Sijali watu wanasema nini. Na—najua. Najua. Naam, bwana. Haijalishi, kama ulimwengu mzima ukisema vinginevyo. "Na—namjua niliyemwamini, na nimeshawishika kuwa anaweza kutunza kile nilichoweka Kwake kwa ajili ya ile siku."

198 Wengi wa marafiki wanaoketi hapa ndani, na kadhalika, baadhi yao huko nje. Nina madaktari marafiki zangu kadhaa waliopo leo, pia.

199 Mimi si mlokole. Ninaninii tu. . .ikiwa inachukua. . . Ukikuita ulokole, kuamini ufufuo wa Yesu, basi mimi ni mlokole. Hiyo ni kweli. Ninaamini hivyo, kwa moyo wangu wote.

200 Sasa, hii hapa hoja yangu, kwamba Yesu alifufuka katika wafu. Ninaamini, kama alifufuka katika wafu. . .Alisema, "Mambo yale yale nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya. Hata zaidi ya haya mtayafanya, kwa kuwa naenda kwa Baba Yangu."

201 Nami naamini, hapa kwenye asubuhi hii ya ufufuo, kama Mungu atatokea tu tena hapa jukwaani, kwa namna ambayo mnaweza kujua kwamba ni Yeye! Je, mngependa kumwona? Je, mngependa kuwa kama Kleopa na hao wengine, wakija? Basi, kama Mungu atafanya hivyo, nimewaambia Kweli ya Injili, basi.

202 Sasa, angefanya nini kama angejitokeza hapa asubuhi ya leo? Angeweza kusema. . .Je, waweza kuja, useme, "Je, utaniokoa, Bwana?"

203 Angesema nini? "Nilifanya hivyo nilipokufa kwa ajili yako pale Kalvari." Maana, hiyo ndiyo Injili Yake.

Useme, "Je, utaniponya, Bwana?"

Angesema, "Nilifanya hivyo nilipokufa kwa ajili yako pale Kalvari."

204 Sasa, jambo pekee ambalo angeweza kufanya, litakuwa ni kuonyesha ishara na maajabu miongoni mwenu, ambayo yangewafanya kuamini na kulikubali. Je, hiyo ni kweli?

205 Sasa, nafikiri hao wavulana walisambaza kadi za maombi asubuhi ya leo. Billy aliniambia, dakika chache zilizopita, kasema, "Ziliisha, katika muda mfupi tu." Lakini hawakuwa na za kutosha kuzunguka. Alikuja apate zingine, na akapoteza wakati wake wa kuja. Alipoanza kutoka nje, kuchukua kadi, ndipo Ndugu Neville akaanza kuimba *Amini Tu*.

206 Na hawa hapa wakaja, wakikimbia kule. Ndipo Ndugu Wood na hao wengine wakasema, "Mbona, nyimbo zilikuwa zimeimbwa tayari, na kadhalika," kwa hivyo ilinibidi kushuka kule mbio. Wala sikutoa kadi nyingi sana, labda hamsini ama mia, kitu kama hicho, pengine. Tunaweza kuwapitia wengi kadiri tuwezavyo.

207 Sasa ninawatakeni mtoe kadi zenu ndogo za maombi. Ni kadi ndogo ya mraba. Inayo picha yangu juu yake, na nyuma yake kuna namba. Nasi tunataka kuwapanga watu, hapa, na kuwaombea, kwa makundi tu wanapokuja. Na tuwaombee kadiri tuwezavyo.

208 Sasa, mnapotoa kadi zenu, na kujitayarisha, sasa nawatakeni mtambue. Kuna wengi hapa ndani ambao hawana kadi za maombi. Huenda ikawa kuna watu mia moja hapa ndani ambao hawana kadi za maombi. Kadi ya maombi haimaanishi chochote, hata kidogo. Kitu pekee inachomaanisha ni wewe umwamini Mungu.

209 Yesu aliwaombea watu, hiyo ni kweli, na mara nyingi angewaambia shida ilikuwa ni nini. Lakini alisema. . .kamwe hakusema, "Nimekuponya." Alisema, "Imani yako imekuokoa." Watu wanaokuja. . .

210 Kulikuwako na yule kipofu Bartimayo, barabarani, ameketi pale, akiombaomba. Yesu akitembea, labda kwenye lango lile, barabara hiyo kutoka—kutoka pale alipokuwa ameketi Bartimayo, ilikuwa kutoka hapa mpaka kwenye ile kona nyingine. Ndipo huyu hapa Yesu anashuka. Na huyo hapo yule ombaomba kipofu ameketi kando ya ukuta pale, akipiga mayowe.

211 Watu wanapiga kelele, "Mwondoeni huyo mlokole! Hima, mropokaji, kwa nini usifanye mwujiza na utuonyeshe!"

212 Wengine wakisema, "Hosana! Hosana! Yeye ndiye Mfalme, wa—wa Daudi, Mwana wa Daudi."

Na wote, tofauti, mchanganyiko.

213 Naye Yesu, akielekea Kalvari, na uso Wake. . .Anaelekea huko. Ninamwona akitembea. Na maisha Yake ya ujana, umri wa miaka thelathini na kitu tu, alionekana mzee. Walisema alikuwa karibu "hamsini," lakini alikuwa na thelathini na mitatu tu. Naye hapo alikuwa ameuweka uso Wake, huku dhambi za ulimwengu zikiwa juu Yake, na kila ugonjwa uliopata kuwako, ukining'inia juu Yake. Naye alikuwa anaelekea Kalvari, kusulubiwa.

214 Ndipo yule maskini mzee ombaomba kipofu pale, mikono michakavu na kila kitu, akisema, "Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu! Nirehemu!"

Watu wakasema, "Keti chini!"

215 Lakini Yesu akasimama; akageuka, akatazama kule nyuma, na akasema, "Imani yako imekuponya." "Imani yako!"

216 Maskini mwanamke mdogo, havutii sana. Akajipenyeza katikati ya umati na chini ya miguu yao, akaenda pale na kugusa vazi Lake, akarudi mbio kule nje kwenye umati mahali fulani na kuketi chini.

217 Yesu akasimama, akasema, "Ni nani aliyenigusa Mimi?" Akatazama pande zote. Akasema, "Imani yako imekuponya."

"Kwa nini kuhoji moyoni mwako?" Kasema . . .

Yule mwanamke kisimani.

Alidhani ilikuwa ni kama ninii-. . .walisema basi . . .

218 Wakati Filipo alipomjia, wakati Yeye. . .mwanzoni mwa huduma Yake. Yesu alikuwa amesimama kwenye mstari wa maombi, akiwaombea wagonjwa.

219 Huyu hapa Yesu, jana. Huyu atakuwa ni Yesu, leo, kwa kuwa ni yeye yule. Wakati hiyo Nuru ilipokuwepo asubuhi, iko hapa jioni, Yesu yeye yule; jana na leo, mnaona, vivyo hivyo tu.

220 Na wakati Yesu alipokuwa amesimama pale, kulikuwako na mtu aliyeokolewa. Alikimbia na kumchukua rafiki yake, aitwaye Nathanaeli. Na kwa hiyo akaenda na kumchukua Nathanaeli. Naye Filipo akaenda akamchukua Nathanaeli. Ndipo akamkuta Nathanaeli chini ya mti, akiomba.

221 Basi alipomrudisha. . .Yesu alikuwa amekuja huko. Akasimama katika kusanyiko, popote alipokuwa. Yesu alikuwa pale, akiwaombea watu.

222 Akatazama nje, akasema, "Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake."

223 "Mbona," akasema, "ulinijuaje, Rabi?" Au, "mwalimu, kasisi," cheo.

224 Akasema, "Mbona, kabla Filipo hajakuita, nilikuona chini ya mti."

225 "Mbona," Mafarisayo wakasema, "mnaona, Yeye ni mpiga ramli. Yeye ni ibilisi. Yeye ni Beelzebuli."

226 Lakini Filipo alisema nini? Nathanaeli alisema nini? Alikimbia kule na kuanguka chini, na kusema, "Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli."

227 Akasema, "Kwa sababu nilikwambia hivi, unaamini? Utaona makubwa kuliko haya, kwa sababu wewe ni mwaminio. Unaona? Utaona makubwa kuliko haya." Mnaona?

228 Sasa, huyo ni Yesu yeye yule leo. Sasa hebu tuwapange wagonjwa, na tuanze kuwaombea.

229 Sasa ninyi huko nje katika wasikilizaji, msio na kadi za maombi, nawatakeni muamini tu kwa moyo wenu wote. Mungu atawaponya, mkiketi moja kwa moja kwenye viti vyenu. Anaweza kuwageuza watumishi Wake na kusema jambo lile lile alilosema wakati huo. Je, hamwamini hivyo? Vema.

230 Sasa nitawaambia ninachotaka mfanye. Nani aliye na kadi ya maombi namba moja? Hebu tuone. Inua mkono wako. Kadi ya maombi namba moja, namba moja. Namba mbili . . .

231 Pangeni mstari *hapa*. Sasa, lazima nichukue tu mmoja kwa wakati mmoja, kwa sababu hatuna . . . ha—hatuna nafasi ya kusimama.

232 Namba mbili, ni nani aliye na kadi ya maombi namba mbili, je, waweza tu kuinua mkono wako? Kadi ya maombi . . . Mama huyu hapa. Namba tatu . . . Njoo huku, upande *huu*, mama. Namba nne, ambaye ana kadi ya maombi . . .

233 Ni nani aliye na kadi ya maombi namba tatu? Siamini kama nimepata hiyo. Kadi ya tatu ya maombi.

Kadi ya nne ya maombi.

234 Kadi ya tano ya maombi. Ni nani aliye na kadi ya tano ya maombi? Mwanamke mmoja huko nyuma. Sawa.

Kadi ya maombi namba sita.

Namba saba.

235 Naomba uje upande *huu*, papa hapa. Sasa hebu, nne, tano, sita, saba. Sijui jinsi gani . . . Wavusheni *huku*, karibu na . . . juu ya jukwaa, labda, pengine. Vema. Haraka tu mwezavyo. Mpiga piano atacheza *Amini Tu*, tafadhali.

Sina njia ya kujua nani, wapi, vipi, lini, nani.

236 Sasa hebu tuone ni wangapi tunaweza kusimamisha. Je, mwaweza kuja moja kwa moja sasa? Hizo ni kadi za maombi namba moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba.

Ni nani aliye na nane, kadi ya maombi nane? Papo hapo, mwanangu.

237 Kadi ya maombi tisa. Inua mkono wako, yeyote aliye na kadi ya maombi tisa.

238 Labda mtu fulani kiziwi, wala hawezi kusikia. Angalia kadi ya mtu anayeketi karibu nawe.

Kadi ya tisa ya maombi, unaweza kuinua mkono wako, tisa?

239 Kuna mtu asiyeweza kusimama? Ikiwa wewe ni kiwete, huwezi kusimama, watakubeba.

Kadi ya tisa ya maombi, labda walitoka nje.

Kadi ya kumi ya maombi. Vema, mama, huku.

Kadi ya maombi kumi na moja. Upande *huo*, bwana.

Kadi ya maombi kumi na mbili. *Huku*, bwana.

Kadi ya maombi kumi na tatu. Vema, mama, *hapa*.

Kadi ya maombi kumi na nne. Hapo, una kumi na nne?

Kumi na tano. *Hapa*, mama, tafadhali.

240 Hiyo ni sawa, njoo tu. Nafikiri ungeenda, labda uzunguke moja kwa moja, ukiweza, kule chini, marefu yale, wewe, tafadhali. Njoo moja kwa moja huko, Bill. Angalau, simama hapa katikati ya marefu hayo. Hiyo ni sawa. Hiyo ni sawa. Wapangishe mstari hapo. Papa *hapa* chini, mama. Mama, papa hapa chini, dada mpendwa. Na upitie moja kwa moja mstarini.

241 Hebu tuone ni wangapi tunaowaweka mstarini. Hebu tungojee kidogo tu, kwenye hawa sasa, kwa dakika moja tu.

242 Sasa iweni tu na uchaji kabisa. Endeleeni kuketi, tulieni, kimya. Sasa, hii ni nyumba ya Mungu. Vema. Chukueni maombi hayo . . .

243 [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Wasemaje? Wasemaje? Sawa, tunaweza kuweka wengine wachache? Sawa. Kadi ya maombi . . .

244 Niliachia wapi? Naam. Kadi yako ya maombi ni ipi, bwana? [Ndugu huyo anasema, "Kumi na nne."—Mh.] Kumi na nne. Sawa.

245 Kadi ya maombi kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini.

246 *Huku*, mama. *Kule* juu, *kule*, nenda *kule*. Vema. Hiyo itafanya takriban idadi tunayoweza kusimamisha. Nenda *huko*, mama. Watakushughulikia, tafadhali. Vema.

247 [Ndugu mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Wasemaje? Vema, hiyo ni sawa. Hao watatosha kadiri tunavyoweza kuwasimamisha sasa hivi, namna hiyo tu.

248 Ati nini? Je, pua ya huyo msichana mdogo inatoka damu, dada? Hebu tusimame tu, dakika chache. Naomba mwinamishe vichwa vyenu kwa muda mfupi tu.

249 Baba, katika Jina la Mtoto Wako mpendwa, Bwana Yesu, tunaomba ya kwamba utamgusa mtoto huyu, Mungu. Ikomeshe damu. Na ikome sasa. Jina Lako na litukuzwe. Kwa maana,

tunakemea mtiririko huu wa damu, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

250 . . .?. . . Vema, hebu na tuendelee kuinamisha vichwa vyetu sasa, kwa dakika moja.

251 Bwana Yesu, katika kusanyiko, leo, kuna wengi wamesimama wakingojea. Tunakushukuru kwa ajili ya nguvu Zako za uponyaji. Sasa tunaomba, kwa moyo wetu wote, Bwana, ya kwamba Wewe utatujalia mambo ambayo tumeomba. Fanya hivyo kwa utukufu wa Mungu. Tunaomba kupitia Jina la Yesu. Amina.

252 Vema, sasa, hebu na tuwe na kicho tuwezavyo. Kumbukeni, sijui. Haya yote ni kusonga mbele tu katika Mungu.

253 Sasa, kuna—kuna watu katika mstari wa maombi ninaowajua. Ndugu Wood amesimama pale, ninamfahamu. Namjua mtu wa pili, wa tatu nyuma ya huyo. Ninawajua. Ninamjua mama huyu anayeketi hapa, mama huyu wa kwanza. Sijui ana shida gani, lakini najua yupo. Nadhani hiyo ni karibu kikomo cha wale ninaowajua katika mstari wa maombi.

254 Kuna wengi hapa ambao—ambao siwajui. Nanyi wenyewe ni mashahidi wa mambo haya, kwamba siwajui ninyi. Lakini Yesu Kristo anawajua, sivyo?

255 Sasa ni wangapi huko nje hawana kadi za maombi, nanyi mnataka kuponywa, kwa vyovyote vile? Inueni mikono yenu, juu kabisa, juu kabisa. Hilo ni sawa. Mungu awabariki, vema, msio na kadi za maombi. Sasa nakuomba ufanye hivi. Kama Roho Mtakatifu akija na kutia mafuta, wewe angalia huku na kuamini kwa moyo wako wote. Uangalie tu, na kusema, "Bwana, hakika ninaamini kwa moyo wangu wote." Kama utafanya hivyo, Mungu atakupa uponyaji wako. "Ninaamini kwa moyo wangu wote." Sasa, msisogee huku na huko. Iweni na kicho kabisa. Iweni tu na kicho kadiri mwezavyo.

Sasa hebu tuombe tena.

256 Sasa nataka kuwauliza, huku vichwa vyenu vimeinamishwa. Ikiwa Yesu amefufuka katika wafu. . . Sasa, huu si wa kukuponya. Huu ni uthibitisho tu kwamba amefufuka katika wafu. Kama Yesu Kristo amefufuka katika wafu, kuhusu wokovu na uponyaji, Yeye tayari ameununua huo pale Kalvari. Hiyo ni kweli? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakuna kitu ambacho angeweza kufanya; ila tu, kufanya kitu, kwa njia ya ishara au maajabu, ambacho kingewafanya kujua kwamba amefufuka katika wafu. Kama angefanya jambo hilo wakati mmoja, mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani, mnapaswa kumkubali. Hiyo ni kweli? Mtafanya hivyo? Kama mtamkubali, inueni mikono yenu. Kama atafanya jambo moja kama alivyofanya alipokuwa

hapa duniani, mtakubali? Mungu awabariki. Asilimia mia mia moja.

257 Sasa, Baba, naomba ya kwamba utakuwa na rehema. Na sasa, kwa ajili ya utukufu Wako, Bwana, ninaomba ya kwamba utalijalia papa hapa, leo, maskanini, ili kulitatua milele, kwamba umefufuka katika wafu. Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba baraka hii kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

258 Sasa, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na kwa Nguvu za kufufuka Kwake, kwa uweza wa Mungu, sasa ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Kwa hivyo, fanyeni jinsi mnavyoambiwa.

259 Na sasa nataka mama huyo, *hapa*, asimame tu papa hapa karibu na maikrofoni. Namjua huyu mama. Na—nafikiri jina lake ni Sutton, sijakose-. . . [Dada huyo anasema, “La. Cobb, sasa.”—Mh.] Loo, Cobb, samahani. Nami nimemwona huyu mwanamke hapo awali, kwa hiyo yeye huja hapa maskanini mara moja moja. Na sasa, bali, sijui chochote kuhusu tatizo lake. Lakini sasa njia pekee ambayo ningekuwa nayo ya kujua jambo hilo, ingekuwa njia fulani ambayo Mungu angekuwa nayo ya kuniambia. Hiyo si ni kweli, Bibi . . . [“Ndiyo, ni kweli.”] Cobb? [“Hiyo ni kweli.”] Cobb? Sawa. Cobb, ingekuwa, ndilo jina lako sasa? [“Ndiyo.”] Sawa.

260 Sawa, Bibi Cobb, njia pekee ambayo ningejua shida uliyo nayo, ingekuwa Mungu ingebidi anifunulie. Na, basi, kama angefanya hivyo, hiyo ingebidi ije kupitia kwa Nguvu za kimbinguni ambazo si za mwanadamu. Ingebidi itoke kwa Nguvu za Kiungu. Hiyo si ni kweli? [Dada huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Na halafu, kwa kufanya hivyo, je, hilo lingekufanya uamini ya kwamba nilikuambia Kweli kuhusu kufufuka Kwake? [“Naam.”] Unaona?

261 Je, itakufanya uamini, rafiki?

262 Sasa, vipi—vipi kama Yesu alikuwa amesimama hapa amevaa suti hii aliyonipa Yeye? Mnaona? Naye—Naye alikuwa amesimama hapa, kama ni . . .

263 Sasa, huyu mwanamke anaweza kuwa na tatizo la kifedha. Anaweza kuwa na matatizo ya nyumbani. Anaweza kuwa na matatizo ya magonjwa. Sijui. Mungu anajua hilo. Sijui. Siwezi kuwaambia. Labda amefanya jambo fulani maishani mwake, ambalo limesababisha kilicho shida yake kumjia. Sijui. Mungu anajua. Sijui mimi.

264 Lakini, anaweza kuniambia. Vema, hivyo ndivyo ilivyo. Yesu alisema, “Sifanyi neno ila Baba anionyeshe.” Haina budi kuja jinsi hiyo.

265 Sasa, ninachomfanyia mwanamke huyu hapa, hakitakuwa ni kusoma mawazo yake. La, bwana. Mungu na aepushe.

Mungu anajua kwamba hilo si kweli. Halitakuwa. Mungu aliye Mbinguni, kama mwamuzi wangu, anajua ya kwamba sivyo. Hilo si sawa, mnaona. Siyasomi mawazo yake.

266 Lakini, itakuwa ni kupitia kwa Nguvu za ufufuo, Yesu Kristo katika Kanisa Lake. Mwangalie Petro na hao wengine, waliposimama pale na kuwatazama hao watu. Jinsi Paulo na watu mbalimbali walivyowatazama watu, nao wakatambua kwamba kulikuwa na mambo fulani ambayo yalikuwa mabaya.

267 Yesu, akiongea na yule mwanamke kisimani, alifanya mazungumzo naye. Sasa, sote tunajua jambo hilo, Yohana Mtakatifu m—mlango wa 4. Alizungumza na yule mwanamke kisimani. Na alipokuwa akiongea na yule mwanamke kisimani, alikuwa akiishika tu roho yake.

268 Baba alikuwa amemwambia apitie njia ya Samaria. Yeriko ndiko alikokuwa anaenda. Ilikuwa ni kushuka moja kwa moja namna *hii*, kutoka Yerusalemu. Bali alizunguka sana huko, akienda Samaria, kwa maana Bwana alimwambia aende kule.

269 Naye akaketi pale kisimani; akawatuma wanafunzi Wake. Alijua huyo mwanamke alikuwa anakuja. Alipokuja na mtungi wake wa maji, Yeye alisema, "Nipe maji ninywe."

Akasema, "Si kawaida Kwako kuniomba kitu kama hicho."

270 Akasema, "Lakini kama ulijua ni Nani uliyekuwa unazungumza naye, ungeniomba Mimi maji unywe. Ningekupa maji ambayo hukuja hapa kuchota."

271 Hiyo ni kweli? Ndipo, baada ya mazungumzo kuendelea kitambo kidogo, hatimaye alipata mahali hasa shida yake ilipokuwa. Kasema, "Nenda kamwite mumeo."

Akasema, "Sina."

272 Kasema, "Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli." Kasema, "Unao watano na yule uliye naye sasa siye mume wako."

273 Akasema, "Naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Ninajua ajapo Masihi Yeye atafanya jambo hili, kwa kuwa atatwambia mambo, lakini u nani Wewe?"

Kasema, "Mimi ninayesema nawe, Ndiye."

274 Sasa, huyo alikuwa ni Yesu jana. Huyo ni Yesu leo.

275 Sasa, ili, kwako, mama, njia pekee niliyo nayo ya kujua, ingebidi kuwe na aina fulani ya mawasiliano kati yako na mimi, pamoja na Mungu, ambayo yangefanya ijulikane.

276 Je, umewahi kuona ile picha waliyopiga ya Malaika wa Bwana akiwa amesimama karibu nami, ile Nuru, wajua? [Dada huyo anasema, "Ndiyo, nimeiona."—Mh.] Wewe, umeona mojawapo ya hizo? ["Nimeiona. Nimeiona."]

277 Je, kanisa limewahi . . . Loo, mmeiona, hapa kanisani, bila shaka.

278 Sasa, Hiyo ndiyo ninayojaribu kuleta karibu nasi sasa. Sasa, Nuru hiyo ndiyo Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, ambayo ilikuwa ni Yesu Kristo, hiyo ni kweli, Malaika wa agano. Yeye alikuwa ni umbo la kimbinguni wakati huo, la Nuru.

279 Alishuka, alikuwa mwili. Akasema, "Nilitoka kwa Mungu, nami ninarudi kwa Mungu."

280 "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona." *Ulimwengu* ni "asiyeamini." "Mtaniona Mimi, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ukamilifu wa dahari."

281 Sasa, Bwana abarikiwe! Na unajua kuwa mimi ni... mimi...jambo fulani linafanyika.

282 Sasa, kwa kusanyiko, ninawatakeni muwe na kicho. Lakini, sasa, Nuru ile ile, Mungu ashukuriwe, inaingia hapa kwenye mkono wangu wa kuume. Inasogea kati yangu na huyu mwanamke. Sasa maisha yake hayangeweza kufichwa.

283 Sasa, dada yangu, Hicho kilicho juu yako sasa si kitu cha kukudhuru. Ni cha kukusaidia. Ndiyo njia pekee ya wokovu. Wewe, uko hapa...

284 La, huishi hapa mjini. Unaishi New Albany. Unaishi New Albany. Nawe uko chini ya—uko chini ya uangalizi wa daktari. Naye huyo daktari amekwambia ya kwamba ni kitu cha aina fulani, kitu fulani kooni. Baadhi...Ni ugonjwa wa kikoromeo kwenye koo lako. Naye alikwambia, na kukushauri, kuondoka humu nchini, uondoke huku, kwamba hiyo ndiyo njia pekee unayoweza kupata nafuu. Je, unaamini ya kwamba Bwana Yesu anaweza kuuponya huu? [Dada huyo anasema, "Ndiyo. Utukufu kwa Mungu."—Mh.]

Na tuinamishe vichwa vyetu.

285 Baba yetu wa Mbinguni, nikiweka mikono juu ya huyu mwanamke, wakati nikiwa katika upako wa Roho Mtakatifu, ninailaani shida hii, ambayo umemponya pale Kalvari, na kuomba kwamba awe huru. Katika Jina la Yesu Kristo ninaomba. Amina.

286 Nenda kwa amani, dada yangu, na Mungu akubariki na awe nawe, ndilo ombi langu.

287 Sasa, Bwana na abarikiwe! Uwe na kicho sasa. Angalia. Mwamini Mungu. Usiwe na shaka.

288 Nataka uangalie huku, mama. Sasa, Yule aliyeko...tuko Mbele Zake, anajua mambo yote, na anakujua tangu mwanzo kabisa. Amekulisha kila kipande cha chakula ambacho umewahi kula. Anajua yote kukuhusu. Huenda nisikujue mimi, lakini Mungu anakujua. Anajua wewe ni nani, unatoka wapi, yote kukuhusu, yale umefanya maishani mwako. Na Yeye Ndiye pekee awezaye kukuponya, ama kukufanyia yale unayotaka kufanyiwa. Unajua kuwa sijui. Mungu pekee ndiye ingembidi

kunifunulia. Je, hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. [Dada huyo anasema, "Ni kweli."—Mh.] Vema, angalia huku kwa muda kidogo tu.

289 Hebu kidogo. Sasa, kila mtu awe na kicho.

290 Huyu hapa Malaika wa Bwana amesimama papa *hapa*, ninii tu . . . Yuko juu ya maskini . . . Yuko juu ya msichana huyu mdogo anayeketi papa hapa. Huyu msichana mdogo yuko pamoja na wapendwa wake. Huyu mtoto anaugua na aina fulani ya ugonjwa kooni mwake. Ni ugonjwa wa koo, ugonjwa wa mafindo. Hiyo ni kweli, sivyo, bwana? Weka mkono wako juu yake.

291 Bwana Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, Shetani amefichuliwa, nami ninamkemea pepo huyo aliyemshikilia huyu msichana.

Toka ndani yake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

292 Ndugu, umetoka mbali, kumleta huyu mtoto, lakini usijali, unampeleka nyumbani sasa apate kuwa mzima, imani yako imekuokoa.

Mwamini Mungu.

293 Wala hutoki Jeffersonville. Umetoka mbali na Jeffersonville. Umetoka mashariki, ukija magharibi, unapokuja hapa. Nawe umetoka . . . umekuja kupitia barabara, ba—barabara ya saruji. Na umetoka katika mji ulio upande wa kulia wa barabara. Ni namna fulani ya shughuli za serikali huko. Ni Edinburgh, Indiana. Umetoka Edinburgh, Indiana. Na jina lako, naona kwenye hilo, ni Denton. Na jina lako, ni Denton. Na unasumbuliwa na ugonjwa wa moyo. Rudi nyumbani ukiwa mzima. Imani yako inakuponya na kukupa afya, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Nenda ukaponywe. Amina. Mungu akubariki.

294 Mwamini Mungu. Amini kwa moyo wako wote. Sasa, kwa hawa watu, iweni na imani! Msiwe na shaka. Aminini tu sasa. Je, mnamwamini? Loo, jamani! Hii, sio mimi; Yeye, Yeye ndiye Yesu aliyefufuka. Yeye ndiye aliye hapa, na kutenda. Haya ni mambo yale yale aliyofanya, hiyo ni kweli, mambo yale yale aliyofanya.

295 Sasa, mama, mimi na wewe tunakutana hapa asubuhi ya leo. Mungu anatujua sote wawili. Sijui chochote kukuhusu wewe. Unafahamu hilo. Lakini Mungu anakujua. Ananijua mimi. Naye Roho wake Yuko hapa kati yetu.

296 Ninataka kukuuliza jambo fulani ili maskani hii ipate kujua. Maishani mwako mwote, hujawahi kujisikia kama unavyojisikia hivi sasa, hiyo ni kweli, kwa sababu uko Mbele ya Utu Wake mweza-yote. Je, umewahi kuona hiyo picha ya Nuru? Hiyo ndiyo hasa inayokufanya ujisikie hivyo.

297 Ninaishi katika ulimwengu mwingine wakati huu. Ninaweza kukuona, natambua tu kuna mtu amesimama mbele yangu. Nawe unajua ni hisia ya upendo, tamu, nyenyekevu. Huyo ndiye

Bwana Yesu aliyefufuka katika wafu. Alirudi kwenye Maisha ya Roho, Mungu. Na sasa Yeye yuko hapa pamoja nasi. Hata ukamilifu wa dahari, Yeye atakuwa pamoja nasi.

298 Wewe ni Mkristo. Wewe ni mwaminio. Wala husimami hapa kwa ajili yako mwenyewe. Unasimama hapa kwa ajili ya mwanamume, na mwanamume huyo ni mume wako. Na mwanamume huyo ana henia. Na jambo lingine, ninamwona, anakunywa pombe kwenye baa. Yeye ni mlevi sugu. Yeye, yeye hunywa. Nawe umekuja kwa ajili ya kukombolewa kwa mtu huyo. Hiyo ni kweli? Sasa unajua, mama, mambo hayo yanapita akili ya mwanadamu yeyote. Hiyo si ni kweli? [Dada huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Hilo halina budi kufunuliwa na Mungu. Unaamini kwa ajili ya huyo sasa? ["Ninaamini."]

299 Mungu Mwenyezi, uliyemfufua Yesu katika wafu, nasi tuko hapa leo tukifurahia baraka za huo ufufuo. Ninambariki huyu, mjakazi Wako, na jalia apokee kile ambacho ameomba. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

300 Mungu akubariki, dada yangu. Nenda, ukapokee chochote kile ulichoomba. Mungu akujalie.

Unaamini?

301 Vema, bwana, niangalie. Namaanisha, sio kuangalia... Namaanisha, kama vile Petro na Yohana walipopitia kwenye lango liitwalo Zuri, wakasema, "Tuangalie." Nadhani hatufahamiani. Hatujuani; labda mara yetu ya kwanza ya kuonana. Je, hii ndiyo ziara yetu ya kwanza, kabisa, wakati wa kuonana? [Ndugu huyo anasema, "Naam."—Mh.] Vema. Basi, sisi hatufahamiani, hatufahamiani kabisa. Sijawahi kukuona, wala wewe hujawahi kuniona. Nasi hapa, wanaume wawili wamekutana hapa maishani. Mungu anatujua sote wawili, sivyo, bwana? ["Anatujua."] Hakika anatujua. Na sasa ikiwa kuna jambo lolote linalokuhusu...

302 Kuna jambo limetokea. Sasa iweni na kicho, kila mtu.

303 Ni mama anayeketi hapa, akiomba, papa *hapa*. Anasumbuliwa na tumbo kuvimba. Simama, kwa dakika moja tu, mama. Hiyo ni kweli, sivyo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Na una msukumo kwenye moyo wako. Si kitu ila kuvimba tumbo, kwa sababu una wasiwasi na kufadhaika. Lakini unaenda nyumbani kupona. Ninaiona nuru ikiingia karibu nawe, ambapo ilikuwa ni giza. Usiogope. Ninii tu...

304 Unaona, huhitaji kadi ya maombi. Kitu pekee unachohitaji ni imani. Mwamini tu Mungu.

305 Mungu akubariki, mama. Amini kwa moyo wako wote.

306 Sasa, pepo mchafu anapoanza kuzunguka sehemu hii *hapa*. Kuna mtu anayeita. Maombi yanafanywa. Ninaona mchirizi mweusi ukitoka kwa mwanamke kwenda kwa mwanaume. Ni kitu kiovu, na kiko chini ya ubavu. Naona uchunguzi. Loo,

ni maskini mtu anayeketi *hapa*, akiomba, akipangusa macho yake. Mungu akubariki, ndugu. Kuwa na imani! Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Unanikubali vivyo hivyo? Sasa, tatizo lile lile ulilo nalo lina mwanamke yule anayeketi pale anayenitazama moja kwa moja mwishoni mwa ile safu, pale pale nje akiwa amevaa kofia ndogo ya mviringo. Kuna mchirizi mweusi. Huyo mama anayeangalia juu ya kichwa cha mama huyu, akiniangalia papa hapa, akiwa ameinua mkono wake. Ndivyo hivyo, mama. Hiyo ni kweli. Huu hapa, ukitoka kwa mmoja ukamwingia mwingine. Ni nguvu za giza, zikivuta; mchirizi mweusi. Una tatizo, liko moja kwa moja chini ya ubavu wako hapa. Ni ugonjwa wa kibofu nyongo. Mama yule pale anao. Ninyi nyote wawili mmeponywa. Yesu Kristo anawaponya. Nguvu hizo chafu zitaondoka, nanyi mtawekwa huru. Amina.

307 Iweni na imani! Sasa, hebu kidogo tu. Roho Mtakatifu yuko kwenye kusanyiko, akifanya kazi na watu huko nje.

308 Mama huyo aliyeinua mikono yake, kuna mama aliyeketi karibu naye, ambaye ninaona uchunguzi wake. Ana shida kwenye njia ya utumbo. Hiyo ni kweli, mama. Je, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Una shida ya matumbo. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako. Je, unamkubali Yesu sasa kama mponyaji wako? Katika Jina la Yesu Kristo Mwana wa Mungu, Yeye aliye hapa kujitambulisha, pokea uponyaji wako katika Jina la Yesu Kristo.

309 Ninamwona mama fulani huku kitu fulani kimezungushiwa kichwani mwake. Inaonekana. . .Loo, ni yule mama anayeketi moja kwa moja nyuma yake, yule mama wa pili anayeketi mle ndani. Anaugua namna fulani ya maumivu ya kichwa. Daima, maumivu ya kichwa. Akitazama niliko mimi. Je, unaamini, mama, unayeketi hapo, maskini mwanamke mwenye mvi, ya kwamba Mungu atakuponya? Je, unaamini kwa moyo wako wote? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Hiyo ni kweli. Mungu akubariki. Yamekwisha. Unaweza kwenda nyumbani sasa. Yalikuacha, papo hapo. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako. Punga mkono wako juu, kama hiyo ni kweli. Umekuacha. Umeponywa.

310 Loo, Jina la Bwana Yesu libarikiwe! Njoo, ukiamini. Roho Mtakatifu akitembea kwenye mstari. Loo, ni ajabu jinsi gani! Je, mnamwamini? Angalieni alichofanya! Laiti ningaliweza kulielezea kanisa langu hisia hii ni nini, jinsi ambavyo, katika ulimwengu mwingine, huna budi kujiuliza kama kweli uko maskanini, au la. Iweni na kicho. Iweni na kicho.

311 Ninaona mtu akija kutoka mbali, mbali sana. Anakuja ma—mahali. Ni mwanaume. Anatoka katika nchi ambamo kuna miti mingi sana. Ni Virginia. Anaugua yabisi kavu. Unaamini Mungu anakuponya na kukupa afya? Unaukubali? Unaukubali? Unatoka Virginia, hapa, ukaponywe yabisi kavu.

Hiyo si ni kweli? Kote kote. . .Naam, bwana. Umeponywa sasa. Unaweza kurudi. Na tatizo lako la moyo limekuacha. Ondoka mstarini urudi nyuma, umepona. Mungu amekuponya. Imani yako imekuokoa.

312 Mwamini Bwana Yesu Kristo! Mnaamini amefufuka katika wafu? Uthibitisho usiokosea wa kufufuka Kwake! Iweni na imani!

313 Sasa, samahani, bwana. Samahani kuwacheleweshа. Si—sina udhibiti wa hili. Inanidhibiti; sio mimi. Inanidhibiti. Naweza kujua ninakuwa dhaifu sana. Lakini najua niko karibu na mtu fulani, mtu mwenye mvi. Sisi ni. . .Najua umevaa miwani. Ambayo, hiyo ingekuwa ni shida uliyo nayo, ingekuwa ni macho yako. Lakini Mungu anajua yote kukuhusu, bwana. Hiyo ni kweli. Uko hapa kuponywa ninii—ninii . . . Una wasiwasi, umefadhaika sana. Imesababishwa na u—ugonjwa wa tezi kibofu. Una tatizo la tezi kibofu. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako. Na pia una ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli. Unao. Pia, tazama, naona ninii yako. . .Sijawahi kukuona maishani mwangu. Lakini herufi zako za mwanzoni ni A. A. Miller. Vema, uko kwenye Mount Valley. Unaelekea nyumbani, upate kuwa mzima. Mungu akubariki. Nenda, ukishangilia, na uamini.

314 Bw. Mills, ni rahisi kwako. Sasa unapaswa kwenda, ukiamini kwa moyo wako wote. Hunijui, sikujui, lakini Mungu anakujua. Je, hiyo ni kweli? Unahisi kwamba kila kitu kimeenda, vema sasa? Mungu akubariki. Nenda nyumbani ukawe mzima.

Kila mmoja wenu!

315 Kwani matone ya moyo ni nini, kwa Mungu? Anaweza kuyaponya wakati wowote. Anaweza kukurudisha Campbellsburg, popote pale, mwanamke mwenye afya njema. Unaamini hilo? Sikujui wewe. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Hunijui. Lakini Yeye anakujua wewe, na kwamba wewe ni nani, na unatoka wapi. Hiyo ni kweli? Amekufunulia. Hiyo ni kweli? Vema, unaamini upako huu ulio juu yangu sasa, ambao unakujua na kila kitu kukuhusu, (sijawahi kukuona hapo awali), kama nikiweka mikono yangu juu yako, utapona? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.]

316 Katika Jina la Yesu Kristo, namkemea huyu ibilisi. Shetani, umefichuliwa. Umewakokota watu hawa kupitia mifereji ya maji machafu kwa muda mrefu kutosha. Toka ndani ya mwanamke huyu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nenda zako, mwenye furaha.

317 Tatizo liko mgongoni mwako, lakini Mungu anaweza kukuponya. Sivyo? Anaweza kukuponya! Unaamini ya kwamba amekuponya? Ikiwa unaamini kwa moyo wako wote! Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ninaukemea ugonjwa

huu. Nenda ukaponywe. Mungu akubariki. Nenda, ukiamini kwa moyo wako wote.

318 Njoo, sivyo. Kwa moyo wako wote, sasa, unaamini? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Hunijui. Sikujui, sijui lolote kukuhusu. Sijawahi kukuona maishani mwangu, nijuavyo mimi. Lakini Mungu Mwenyezi anakujua. Sivyo? Anajua yote kukuhusu. Anajua wewe ni nani, anajua kila kitu. Sijui, sina njia ya kujua, lakini Yeye anajua. Lakini je, unaamini ya kwamba unasimama Uweponi, si mwa ndugu yako, bali mwake Yeye aliyemwangalia yule mwanamke na kumwambia shida yake ilikuwa wapi? ["Ndiyo."] Ninaona, kati yako na mimi inakuja meza, nawe unasonga mbali nayo. Una shida ya tumbo. Ambayo imetokana na donda la mmeng'enyo tumboni. Sasa nenda ukale chakula chako cha jioni. Yesu Kristo anakuponya. Nenda, ukiamini kwa moyo wako wote.

319 Njoo, jamaa mdogo. Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? [Ndugu huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.] Kwa nafsi yako yote, unalikubali? Sikujui, bali Mungu anakujua. Hiyo si ni kweli? ["Naam. Hiyo ni kweli."] Unataka kuondokana na tatizo la moyo na kuponywa? ["Naam."] Vema, nenda zako, ukishangilia. Imani yako inakufanya mzima, inakuponya na kukupa afya.

320 Utakuja, ewe mama? Ulikuwa na tatizo la tumbo, pia. Na wakati mama yule alipoponywa dakika chache tu zilizopita, ugonjwa wa tumbo, hisia ya ajabu kweli ilikuja juu yako, sivyo? Uliponywa, wakati uo huo. Nenda zako, na ule chakula chako cha jioni, na upate afya.

321 Nataka kusema jambo fulani, ndugu yangu. Mungu anakujua. Kati yako na mimi kimesimama kivuli cheusi. Ni ugonjwa unaoua watu wengi kuliko kitu kingine chochote. Ni tatizo la moyo. Moyo wako unavuja, nao wanakwambia kuwa huwezi kupona. Lakini Mungu anajua kwamba unaweza. Je, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya sasa hivi? [Ndugu huyo anasema, "Naam."—Mh.] Katika Jina la Yesu Kristo, pokea uponyaji wako, na uondoke kwenye jukwaa hili ukiwa mtu mzima. Nenda, ukimpa Mungu sifa na utukufu!

322 Ulikuwa na tatizo lile lile. Lililosababishwa na moyo wenye fadhaa, hata hivyo, hali yako. Hiyo ni kweli. Sasa unaamini ya kwamba umeponywa? Basi rudi nyumbani kwako, ukishangilia, na uwe mzima kwa utukufu wa Mungu.

323 Angalia hapa, mama. Unaamini? Hebu kidogo. Hatufahamiani. Hatujuani.

324 Lakini kuna mshtuko wa kutisha uliotoka jukwaani, ama, kwa umma, wakati huyu mama alipokuja hapa. Loo, uko kote juu ya kusanyiko.

325 Angalia huku, kwa dakika moja tu. Unajua, mama, mimi kutokukuona maishani mwangu, sijui lolote kukuhusu. Mungu Pekee ndiye anayekujua. Lakini, ninakuona, u—umefadhaika sana. Ni fadhaa. Umerukwa na akili, nawe u—unaangusha vitu kila wakati. Ninakuona ukiangusha vyombo na kadhalika. Nawe ulikuwa ukiomba, kabla tu hujaja hapa, kwenye kiti, ukiketi karibu na sakafu. Nawe ulimwomba Mungu, kama ungeweza kufika hapa nami nikuwekee mikono, ungepona. Hiyo ni kweli. Sivyo? Inua mikono yako. Hiyo ni kweli.

Ni pepo. Kitu hicho kiko juu ya kusanyiko.

326 Maskini yule mama anayeketi pale *pale*, mwalimu wa Biblia, anayeketi pale akiteseka na jambo lile lile. Ibilisi anakudanganya, mama. Uko tayari kukombolewa.

327 Angalia pale, kote jengoni, hapa, kila mahali. Huyu hapa ameketi mwingine papa *hapa*. *Kuna* mmoja pale pale. Huyu *hapa* mwingine. Loo!

328 Kila mmoja wenu aliye na shida ya fadhaa, simama kwa miguu yako kwa dakika moja. Tafadhali, simama kwa miguu yako.

Sasa inamisha kichwa chako, kila mtu.

329 Loo, Shetani, wewe pepo mchafu! Umefichuliwa. Toka kwa watu hawa. Ninakukemea, katika Jina la Yesu Kristo. Waache watu hawa. Toka.

330 Angalia hapa sasa, mama. Hebu kidogo. Sasa uko huru. Yote yamekuacha. Nataka kuuliza . . . Kila mmoja wenu ameponywa. Ninyi kundi lote mmeponywa. Yule mwovu amekuacha. Sasa unajisikia mtulivu sana. Uko sawa sasa. Sasa nenda zako, kwa furaha, ukishangilia, ukimshukuru Mungu kwa ajili yake. Vema.

331 Njoo, bwana. Mimi na wewe hatufahamiani. Hatujuani. Sijawahi kukuona, maishani mwangu. Mungu anakujua. Angalia hapa, bwana. Niangalie tu kwa muda kidogo tu.

332 Sasa, kwa kusanyiko. Huyu hapa mgeni. Sijawahi kumwona huyu mtu. Simjui, sijawahi kumwona. Mungu anajua hilo. Kadiri nijuavyo, sijawahi kumwona, maishani mwangu.

333 Lakini ninatangaza kwamba Yesu alifufuka katika wafu, kwamba mambo yale yale ambayo Yesu alifanya alipokuwa hapa katika—katika mwili ambao ungeweza kuuona, yuko papa hapa leo akifanya jambo lile lile. Amefufuka katika wafu, na yu hai hata milele. Heri macho yenu myaonayo mambo haya na kumwamini Bwana Yesu!

334 Mtu huyu, mgeni. Sijawahi kumwona, na labda hajawahi kuniona. Ikiwa nimeninii . . . Ikiwa nimewahi kumwona, Mungu anajua sikumbuki. Alisema simjui. Lakini Mungu anamjua. Kama Mungu atafunua, kwa mtu huyo aliyesimama hapo, mgeni kabisa kwangu, ana shida gani hasa, yote kuhusu hiyo; amwambie shida yake, chochote ilicho, naye anajua kuwa sijui

lolote kuihusu, mtamkubali Kristo kama mponyaji wenu, kila mmoja wenu?

335 Jengo limeanza kufifia na kurudi. Laiti mngalitambua tu sababu ya mimi kuzungumza nanyi, enyi marafiki! Unaingia katika ulimwengu mwingine. Uko mahali pengine. Uko chini kabisa ya mkondo wa wakati, katika maisha ya mtu fulani, ukiwaona, kwamba wao ni nani na wako wapi. Hutambui. Ninatambua haifanyi, haifanyi kazi kikamilifu humu ndani, kwa sababu ni nyumbani. Hiyo ni kweli. Lakini mnaona kwamba amefufuka katika wafu. Mnaona kwamba nimewaambia ukweli.

336 Sasa niangalie, bwana, kwa dakika moja tu, kusudi mimi na wewe tuweze kuwasiliana na Bwana Yesu. Ikiwa mimi ni mtumishi Wake, Yesu alisema, "Mambo nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya."

337 "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena," huyo ni asiyeamini. Wako huko nje kwenye michezo ya mpira na kuogelea, na kadhalika. Hawatamwona kamwe.

338 "Bali ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari."

339 Basi, kama amefufuka katika wafu, Naye amesimama hapa asubuhi ya leo, na upako huu nilio nao sasa si wangu, bali ni Wake. Basi usingeweza kuyaficha maisha yako hata ufanye nini, kwa sababu tunawasiliana sisi kwa sisi, kwa Utu wa Roho. Ikiwa Mungu anaweza kunifunulia kilichokufanya usimame hapo, utaikubali kwa moyo wako wote? [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Utaikubali? ["Naam, bwana."]

340 Unasumbuliwa na tumbo. Hiyo ni kweli kabisa. Na sababu yake, ni kwa sababu wewe ni . . . Imesababishwa na ugonjwa wa fadhaa. Wala sio wasiwasi, wa nje, wasiwasi wa kutetemeka. Naona wewe ni mtu wa mawazo mazito. Daima unapanga kitu, ukivuka madaraja kabla hujayafikia kamwe. Unafanya mambo ambayo hayatimii, nawe umeambiwa hivyo hapo awali. Hiyo ni kweli. Lakini haiwafaidi kitu kukwambia, kwa sababu . . . Lakini sasa itawafaidi, kwa sababu umeponywa. Unaenda nyumbani mtu mwenye afya. Yesu Kristo amekuponya.

341 Katika Jina la Yesu Kristo Mwana wa Mungu, ninakemea kila pepo mchafu anayemsumbua mtu huyu. Basi jalia aende kwa amani, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki.

342 Je, mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Moyo wenu wote? ["Amina."] Je, mnaamini Yesu Kristo alifufuka siku ya Pasaka? ["Amina."] Je, mnaamini Uwepo Wake upo hapa sasa? ["Amina."] Je, mtanitii mimi kama nabii Wake? ["Amina."] Ikiwa mtafanya hivyo, vivyo hivyo, kila mmoja wenu anaweza kuponywa sasa hivi. Kila mtu hapa ndani anaweza kuponywa. Je, mnaamini hilo? ["Amina."] Basi inamisha kichwa chako.

343 Mungu Mwenyezi, mwanzilishi wa Uzima, mpaji wa kila karama, tuma baraka Zako za Kiungu juu ya wasikilizaji hawa. Na sasa Roho Wako anaposonga mbele, na kusanyiko hili hapa katika hali hii, ninakemea kila pepo mchafu, kila pepo ambaye amewafunga wagonjwa. Kristo yuko hapa, Yeye aliyefungua milango na kuwaweka huru mateka, na kila mmoja wao yuko huru kwa sababu Yesu alifufuka katika wafu na anajithibitisha Mwenyewe hapa leo.

Shetani, ondoka kwa hawa watu, katika Jina la Yesu Kristo.

344 Basi hebu kila mtu anayeamini sasa, sijali ni hali ipi, ninyi kwenye mikongojo hapo, simameni, kila mtu asimame, katika Jina la Yesu Kristo, na apate afya na kuponywa.

55-0410M Thibitisho La Kufufuka Kwake
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org